# Pambazuko

Toleo Namba 167 | Jumatatu, Juni 1-7, 2026



# Ahadi za Samia zamtesa Ulega



**AHADI za ujenzi wa barabara ambazo zimewahi kutolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia ilani yake ya uchaguzi 2025, zimegeuka kuwa mwiba mkali kwa Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega.**

Uk. 6&7

**Na mshindi ni...**




*Mwandishi Bora wa Tanzania – 2025, Simon Martha Mkina akiwa na tuzo tatu alizonyakua kwenye Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT) Ijumaa iliyopita. Hafla ya tuzo hizo zinazotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) zilishindanishwa kazi 594 za kihabari. (Picha na Comfort Ritha).*

# Ni Mkina, Mwandishi Bora Tanzania

Uk. 12&13

## Mzee adai mtoto wake kamtupa porini

Habari Uk. 16

## Ukatili wa Mahita gumzo



**BAADHI ya watu wamemtaka aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Omari Mahita kuomba radhi Watanzania.....**

Habari Uk. 20

### Jicho la Tai

## Mheshimiwa akitukana, raia ashukuru?

**KUNA ugonjwa mpya unaomea taratibu kwenye baadhi ya vinywa vya viongozi wetu.**

Safu Uk. 5

## Wizara yakwepa hoja vikwazo vya Marekani

Uk. 23

## Tahariri

# Kongole MCT kwa umakini kuheshimisha uandishi

HAFLA ya tuzo za uandishi wa habari iliyoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) Ijumaa iliyopita jijini Dar es Salaam haikuwa tukio la kawaida la kugawa vyeti, vikombe na pongezi zingine.

Ilikuwa ni jukwaa muhimu la kuthibitisha kuwa taaluma ya habari nchini bado ina watu, taasisi na wadau wanaothamini kazi ya waandishi wa habari kwa kina, kwa weledi na kwa heshima inayostahili.

Pambazuko tunachukua fursa hii kulipongeza Baraza la Habari Tanzania kwa kuandaa hafla yenye hadhi hiyo ya kimataifa kwa umakini mkubwa.

MCT imethibitisha kwa vitendo kuwa inatambua nafasi ya vyombo vya habari katika kujenga taifa lenye mijadala yenye afya, wananchi wenye taarifa sahihi na uongozi unaowajibika.

Katika mazingira ambayo uandishi wa habari unakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo ushindani wa taarifa zisizothibitishwa, shinikizo la kibiashara, mabadiliko ya teknolojia na wakati mwingine mazingira magumu ya kazi, hatua ya kuwatambua waandishi mahiri ni ya kupigiwa mfano.

Tuzo hizi zina maana pana kuliko furaha ya mshindi mmoja mmoja. Zinatoa ujumbe kwa tasnia nzima kuwa kazi bora inaonekana, inathaminiwa na inaweza kuwa chachu ya kizazi kipya cha waandishi wanaoamini katika utafiti, ukweli, maadili na maslahi ya umma.

Mwandishi anapotambuliwa kwa kazi yake, siyo yeye pekee anayeshinda; jamii nzima inanufaika kwa sababu tuzo hizo huhamasisha uandishi wenye tija, kina, uwajibikaji na ujasiri wa kuandika habari zinazosukumwa na maswali magumu kwa manufaa ya wananchi.

Tunawapongeza washindi wote wa nafasi mbalimbali. Kila mmoja aliyepanda jukwaani kubeba tuzo amebeba pia heshima ya taaluma hii. Tunawapongeza pia walioteuliwa, kwani kufika katika hatua hiyo ni ushahidi kuwa kazi zao ziligusa viwango vya juu vya ushindani na ubora.

Kwa pamoja, washindi na washiriki wote wameonyesha kuwa Tanzania ina hazina kubwa ya waandishi wenye vipaji, bidii na uwezo wa kuchangia mageuzi chanya ya kijamii.

Kwa namna ya pekee, Pambazuko tunayo fahari kubwa kumpongeza mshindi wa jumla ambaye anatoka katika gazeti hili – Simon Martha Mkina, ambaye ni mhariri mkuu.

Ushindi huu ni heshima kwa chombo chetu, lakini pia ni uthibitisho wa msimamo wetu katika kuendeleza uandishi wa tija, wenye hadhi na unaozingatia weledi na matakwa ya uwajibikaji, uchambuzi makini na habari zinazobeba maslahi ya umma.

Tunaipokea heshima hii kwa unyenyekevu, tukitambua kuwa tuzo siyo mwisho wa safari, bali ni deni jipya la kuendelea kufanya vizuri zaidi.

MCT imeonyesha njia, sasa ni wajibu wa vyombo vya habari, wahariri na waandishi kuendeleza viwango vya juu vya utendaji, kuwekeza katika mafunzo, kuzingatia maadili, ubunifu na ujasiri wa kitaaluma.

Taaluma ya habari ikiheshimiwa, taifa hufaidika na waandishi wakitambuliwa, ukweli hupata nguvu zaidi.

# Mazingira



*Majitaka yanayotiririshwa kwenye mtaro wa wazi wa kupitisha maji ya mvua kwenye Mto Ng'ombe kama yalivyokutwa na kamera ya Pambazuko jana. Hali hii ni hatari kwa afya za wakazi wa eneo hilo la Mwananyamala, Dar es Salaam. (Na Mpigapicha Wetu)*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

***Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz***

# Jaji Kayobera, Sungura wahimiza vyombo huru vya habari

Na Mwandishi WETU



Jaji Nestori Kayobera

VYOMBO huru vya habari, vinavyofanya kazi zake kwa kuzingatia weledi, ni muhimu katika kusukuma mbele maendeleo ya kiuchumi na utoaji haki.

Hayo yameelezwa na Rais wa Mahakama ya Afrika Mashariki, Jaji Nestori Kayobera katika hotuba yake wakati wa sherehe za Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) zilizoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Tuzo hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam na kushuhudia Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Martha Mkina, akitangazwa kuwa Mwandishi Bora wa Habari Tanzania kwa mwaka 2025.

Jaji Kayobera alisisitiza kuwa waandishi wa habari wana nafasi kubwa katika kulinda haki, utawala bora na demokrasia siyo hapa nchini tu bali ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki.

Alibainisha kwamba ingawa mhimili wa kutoa haki, lakini mahakama haiwezi kutoa haki bila ukweli, huku ukweli huo ukiutegemea uandishi wa habari wenye maadili.

Jaji huyo alisema waandishi wa habari ni nguzo muhimu katika kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi zinazowasaidia kushiriki katika maendeleo ya jamii na usimamizi wa haki.

"Mahakama haiwezi kutoa haki bila ukweli, na ukweli hauwezi kufika mahakamani bila mwandishi wa habari mwenye maadili…"

"Waandishi wa habari siyo wageni katika ukumbi wa haki, ni mashahidi wakuu wa jamii na walinzi wa mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema.

Alisema ndiyo maana hata Mkataba wa Jumuia ya Afrika Mashariki imeweka kinga kwa vyombo vya habari kupitia ibara ya sita inayozitaka nchi wanachama kulinda misingi ya utawala bora, ikiwemo uhuru wa kujieleza.

Jaji Kayobera alisema wananchi hawawezi kushiriki kikamilifu katika maendeleo bila kupata habari sahihi na za kuaminika.

Aliwataka waandishi wa habari kuzingatia kanuni tatu muhimu za uandishi bora ambazo ni ukweli uliothibitishwa, maslahi ya umma na kulinda utu wa binadamu.

Alisema kama ilivyo mahakamani ambapo anayetoa madai hutakiwa kuthibitisha, ndivyo ilivyo kwa mwandishi wa habari anayetakiwa kuhakikisha taarifa anazochapisha zimethibitishwa.

Aidha, alieleza kuwa sekta ya habari ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kuenea kwa habari za uongo, pamoja na changamoto mpya zinazoletwa na teknolojia na akili mnemba.

Alisisitiza kuwa changamoto hizo zinahitaji ushirikiano wa pamoja kati ya serikali, taasisi za habari na vyombo vya kujidhibiti ili kuimarisha taaluma ya habari na kulinda maadili ya kazi hiyo.

Inaendelea Uk. 15

Na Mzee TAI



# Mheshimiwa akitukana, raia ashukuru?

**Mawasiliano ya uongozi yanahitaji hekima. Kiongozi asiyekuwa na busara hugeuza swali kuwa uhasama. Hageuzi ukosoaji kuwa vita. Hageuzi tofauti ya mawazo kuwa sababu ya kumdhalilisha raia. Uongozi siyo kipaza sauti cha kuwatisha watu; ni daraja la kusikiliza, kueleza na kujenga imani.**

KUNA ugonjwa mpya unaomea taratibu kwenye baadhi ya vinywa vya viongozi wetu. Siyo kikohozi, siyo mafua, wala siyo homa.

Ni ugonjwa wa madaraka kuingia kichwani na kutoka mdomoni kama kejeli, dharau na wakati mwingine maneno yanayofanana kabisa na matusi.

Ajabu ni kwamba ugonjwa huu huwapata zaidi watu waliokula kiapo cha kuwatumikia wananchi.

Siku hizi, mwananchi akiuliza swali, anaambiwa hana uelewa. Akihoji huduma, anaambiwa anachochea. Akiikosoa serikali, anaonekana adui wa maendeleo. Akiuliza kuhusu maji, barabara, dawa hospitalini au fedha za umma, ghafla anapewa somo refu la uzalendo, kana kwamba uzalendo ni kukaa kimya hata ukiwa na kiu.

Baadhi ya viongozi hawa wamejenga tabia ya ajabu sana. Wao wakizungumza kwa sauti, huo ni msimamo. Mwananchi akizungumza kwa sauti, huo ni uchochezi. Wao wakikosoa waliopita madarakani, huo ni uchambuzi. Mwananchi akikosoa waliopo madarakani, huo ni utovu wa nidhamu.

Hapo ndipo unagundua kuwa katika nchi zetu, amani na demokrasia hutamkwa na wakubwa wetu na kuonekana kuwa na maana zaidi, lakini kumbe wanapozungumza haya ni kama wanavaa koti kubwa, lakini ndani yake wameficha mapanga na bunduki.

Viongozi wetu wengi wanaamini kuwa wananchi wanapaswa kupongeza uvumbuzi huu mpya; kwamba kiongozi kumtukana mwananchi, kisha mwananchi anatakiwa apige makofi.

Hii tabia ikiachwa ikamea zaidi, haitakuwa tofauti na dhana hii; kwamba daktari amzabe kibao mgonjwa kwa sababu ameuliza dawa ina madhara gani. Au mwalimu kumfukuza mwanafunzi darasani kwa sababu ameuliza swali gumu.

Tukilea viongozi wa namna hii, tusishangae kufika mahali tutakwama kwani tutakuwa tumelea falsafa mpya ya baadhi ya wenye madaraka; kwamba usiulize, shangilia; usikosoe, sifia; usifikiri, kubali.

Lakini ukweli ni kwamba, serikali siyo nyumba ya mtu binafsi. Ni taasisi ya umma. Viongozi siyo mabwana wa wananchi; ni watumishi wao.

Kodi inayolipa mishahara, magari, mafuta, posho na ofisi nzuri haitoki mbinguni. Inatoka kwa wananchi haohao wanaoitwa wasumbufu wanapohoji.

Mawasiliano ya uongozi yanahitaji hekima. Kiongozi asiyekuwa na busara hugeuza swali kuwa uhasama. Hageuzi ukosoaji kuwa vita. Hageuzi tofauti ya mawazo kuwa sababu ya kumdhalilisha raia. Uongozi siyo kipaza sauti cha kuwatisha watu; ni daraja la kusikiliza, kueleza na kujenga imani.

Wananchi hawahitaji viongozi wanaowabembeleza kwa uongo. Wanahitaji viongozi wanaowaheshimu kwa ukweli. Kukosolewa siyo kudharauliwa. Na kutofautiana kimtazamo na imani, siyo uadui.

Kwa hiyo, wale viongozi wanaodhani maneno makali ndiyo uimara wa uongozi, wajue kuwa historia ina kumbukumbu ndefu kuliko hotuba zao.

Madaraka hupita. Vyeo huisha, lakini namna ulivyowasema wananchi wako hubaki kama alama kwenye ukuta.

Kiongozi anayewatukana wananchi wake, hata akivaa suti nzuri kiasi gani, hukumbukwa zaidi kwa kuvaa dharau.

# Ahadi za Samia zamtesa Ulega



*Rais Samia Suluhu Hassan*

**Na Mwandishi WETU, DODOMA**

AHADI za ujenzi wa barabara ambazo zimewahi kutolewa na Rais Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia ilani yake ya uchaguzi 2025, zimegeuka kuwa mwiba mkali kwa Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega.

Ulega alijikuta katika wakati mgumu wiki iliyopita mara baada ya kuwasilisha bajeti ya wizara yake kwani Kamati ya Miundombinu na baadhi ya wabunge walikuja juu wakihoji mambo mbalimbali ndani ya wizara hiyo nyeti.

Kati ya vitu ambavyo wabunge walihoji ni ucheleweshwaji wa ujenzi wa barabara zilizoahidiwa na Rais Samia na Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Pamoja na kuchelewa kwa ujenzi wa barabara hizo zilizoahidiwa, Ulega pia alijikuta katika hali ngumu pale kamati na wabunge walipokataa pendekezo la serikali kutaka kuchukua sehemu ya fedha za mfuko wa barabara na kuzihamishia kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Akizungumza baada ya Ulega kuwasilisha bajeti hiyo ya zaidi ya shilingi trilioni mbili, Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Moshi Kakoso alisema kuchukua fedha za Mfuko wa Barabara na kuzipeleka eneo jingine ni uvunjaji wa waziwazi wa sheria.

Akifafanua, Kakoso alisema fedha hizo zimetengwa na kuwekewa kinga (ring-fenced) ikimaanisha kuwa haziwezi kuhamishwa na kupelekwa sehemu nyingine bila sheria hiyo kufutwa.

Akaieleza serikali kuwa iwapo itazichukua fedha hizo basi itakuwa imevunja sheria ambayo imetungwa na Bunge.

Akasema iwapo serikali itataka kuzichukua fedha hizo na kuzihamishia eneo jingine basi kwanza ipeleke bungeni mabadiliko ya sheria iliyoweka kinga kwa fedha hizo za Mfuko wa Barabara.

**Mfuko wa Barabara**

Katika taarifa yake, Kamati ya Miundombinu ilionyesha kutoridhishwa na mtiririko wa fedha za Mfuko wa Barabara.

Kamati hiyo ilibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2025/26 Bodi ya Mfuko wa Barabara, iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 945.794 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara nchini.

"Hata hivyo, kamati ilibaini kwamba hadi kufikia tarehe 24 Machi, 2026 kiasi cha shilingi bilioni 418.876 pekee, sawa na asilimia 44 tu ya bajeti ya bodi ndiyo kilikuwa kimehamishiwa katika akaunti za Mfuko…"

"Kamati inalikumbusha bunge lako kuwa, fedha za Mfuko wa Barabara ni fedha zinazolindwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, serikali kushindwa kuhamisha fedha hizo katika akaunti ya Mfuko wa Barabara kwa wakati, inachelewesha matengenezo na ukarabati wa barabara nchini ambazo zimeathirika na hali ya mvua nyingi,"alisema Kakoso.

Inaendelea Uk.7

# Ahadi za Samia...

Inatoka Uk. 6

Kakoso akasema kuwa hali hiyo pia imekuwa ikiripotiwa karibu kila mwaka na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) bila serikali kuchukua hatua ya kuirekebisha.

Aidha, Kamati ililieleza Bunge kuwa imebaini kuwa serikali ina mpango wa kuchukua asilimia tano ya fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kugharamia miradi mingine ya maendeleo.

“Pamoja na nia njema ya serikali, kamati haikubaliani na uamuzi huo na inaliomba bunge lako kuiunga mkono kwa ajili ya kunusuru sekta ya barabara nchini...”

“Hii inatokana na ukweli kuwa, mahitaji ya fedha katika kufanya matengenezo na kukarabati barabara na maradaja nchini ni makubwa na kuliko kiasi cha fedha kinachopatikana,” alisema Kakoso na kubainisha kuwa uamuzi huo utapunguza ufanisi na tija katika kukabiliana na ubovu pamoja na uchakavu wa miundombinu ya barabara na madaraja nchini.

**Wabunge waja juu**

Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, aliungana na kamati hiyo akishangaa ni kwa vipi serikali inataka kuvunja sheria iliyotungwa na bunge hilo na kuchukua fedha kutoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Nape pia alikuwa mmoja wa wabunge walioiwekea ngumu bajeti hiyo kutokana na kile alichokiita serikali kudharau ujenzi wa barabara inayoelekea mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara.

Nape aliliambia bunge hilo kuwa haiungi mkono bajeti hiyo huku akionyesha dhamira ya kushikilia shilingi kutokana na serikali kutojali kilio cha watu wa kusini kuhusiana na barabara.

Alisema kuwa barabara inayounganisha mikoa hiyo na Dar es Salaam (Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mtwara) ilishafikia mwisho wa muda wake wa matumizi hivyo kuendelea kuikarabati ni kupoteza muda na fedha. Alisisitiza kuwa barabara hiyo inahitaji kujengwa upya.



Waziri Abdallah Ulega

“Barabara hii imezibwa viraka mpaka sasa hakuna pa kuweka kiraka kipya. Hii barabara inatakiwa kujengwa upya kwa sababu muda wake wa matumizi ulishamalizika zamani,” alisema Nape.

Mbunge huyo aliyewahi kuwa waziri alionesha kushangazwa na barabara hiyo kuelekea mikoa ya kusini kutokuwepo kwenye bajeti licha ya ujenzi wake kuahidiwa na Rais Samia na pia kuingizwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Nape alieleza pia kushangazwa kwake na barabara hiyo kutoingizwa kwenye bajeti licha ya mikoa hiyo kuchangia dola za Marekani milioni 580 katika pato la taifa kupitia mauzo ya korosho msimu uliopita.

“Hii barabara ni mbovu sana. Muda wake wa matumizi umepita, wameziba mpaka hakuna sehemu ya kuziba. Nimesoma randama mara nne na sijaiona barabara hii katika bajeti. Mimi siiungi mkono bajeti hii kwa sababu nikiiunga mkono nitakuwa nawasaliti wananchi wa kusini,” alisema Nape.

Inaendelea Uk.8

# Ahadi za Samia...

Inatoka Uk. 7

> **Kwa hakika hakuna mwekezaji binafsi ambaye atakataa kuwekeza kwenye barabara inayopitisha malori 10,000 kwa siku kwa sababu anajua kuwa fedha zake ni lazima zitarudi," alisema Kakoso.**

Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timetheo Mnzava, naye aliipinga bajeti hiyo akidai ujenzi wa barabara ya Handeni-Kibirashi hadi Singida na barabara nyingine kadhaa ambazo ziliahidiwa na Rais Samia.

Akizungumza kama mbunge baada ya kuwasilisha ripoti ya kamati, Kakoso, ambaye ni mbunge wa Mpanda Vijijini, alisema tatizo kubwa linaloikabili wizara hiyo ni uchache wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Aliwaambia wabunge wenzake kuwa watakasirika sana lakini matatizo yao hayatakwisha kwa kushika shilingi kwani fedha zilizotengwa kwa ajili ya wizara hiyo ni chache sana ukilinganisha na mahitaji ya barabara nchini.

Akaishauri wizara hiyo kujikita kwenye mpango wa kuishirikisha sekta binafsi (PPP) katika ujenzi wa barabara.

"Kwa hakika hakuna mwekezaji binafsi ambaye atakataa kuwekeza kwenye barabara inayopitisha malori 10,000 kwa siku kwa sababu anajua kuwa fedha zake ni lazima zitarudi,"alisema Kakoso.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Kasheku Musukuma, aliwataka wabunge wenzake wasiipitishe bajeti hiyo ili kutoa somo kwa serikali kwa kila kinachofanyika kupitia wizara hiyo.

### Janga la taifa

Itakumbukwa kuwa takribani wiki tano zilizopita, wakati akichangia hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mbunge wa Kigoma Mjini, Clayton Chipando, almaarufu Baba Levo, aliishauri serikali kutangaza matatizo ya barabara nchini kuwa janga la taifa.

Alibainisha kuwa asilimia zaidi ya 90 ya wabunge walioijadili hotuba hiyo ya Ofisi ya Waziri Mkuu walilalamika kuhusu ubovu wa barabara katika maeneo yao, hali inayotoa picha kuwa hilo ni tatizo lililoenea karibu nchi nzima.

Naye akasisitiza kuwa barabara ni muhimu kwani masuala mengine ya maendeleo yanayofanyika kama hakutakuwa na barabara basi yatakuwa kazi bure.

"Kwa mfano ukifikisha mbolea kwa mkulima, akalima na kuvuna, kama hakutakuwa na barabara ya kupitisha mazao yake kwenda sokoni basi hiyo ni kazi bure. Kama utajenga hospitali halafu hakuna barabara ya kupitisha ambulance ili kuwafikisha wagonjwa hiyo nayo ni kazi bure," alisema Baba Levo.

### Bajeti yenyewe

Katika bajeti hiyo Waziri Ulega aliliomba bunge liidhinishe shilingi trilioni 2.564 kwa ajili ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

Ulega alivitaja baadhi ya vipaumbele vya wizara katika mwaka ujao wa fedha kuwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara za kupunguza

msongamano hususan katika majiji na miji inayokua kwa kasi.

Alisema mipango hiyo itatekelezwa katika majiji ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya.

Kipaumbele kingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara zinazounganisha makao makuu ya mikoa, Tanzania na nchi jirani na maeneo ya kimkakati.

Aidha, kipaumbele kingine ni kuendelea na ukarabati na matengenezo makubwa ya maeneo yenye changamoto katika barabara kuu na za mikoa na kuendelea na kuimarisha usafiri na miundombinu ya vivuko.

Ulega aliliambia Bunge pia kuwa fedha hizo zitatumika kuendelea kuwajengea uwezo wataalam na wakandarasi wa ndani katika masuala ya ujenzi na pia kuendelea na ujenzi wa majengo ya serikali na nyumba za gharama nafuu.

Licha ya malalamiko ya wabunge hao, lakini bunge liliipitisha bajeti hiyo baada ya mjadala uliodumu kwa siku mbili.

# Pambazuko lang'ara




*Mwandishi Bora wa Tanzania – 2025, Simon Martha Mkina wa Gazeti la Pambazuko katika picha tofauti wakati wa hafla ya Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari (EJAT).*









*Jackton Mayerere wa Gazeti la Jamhuri akipokea cheti baada ya kutangazwa mshindi wa Mhariri Bora wa 2025.*



## Ujumbe Muhimu





Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



# Lugha ya viongozi na afya ya taifa

LUGHA na jinsi inavyotumika ni muhimu sana hasa kwa viongozi wa aina yoyote. Lugha inavyotumika huweza kujenga na kuzua taharuki na hata kubomoa.

Lugha ya viongozi ni zaidi ya maneno yanayotamkwa, kutokana na dhima wanayobeba kwenye jamii.

Lugha huweza kujenga matumaini, kuleta huzuni, kugawa na hata kuimarisha demokrasia.

Jamii huwa inathamini viongozi wake siyo kutokana na mamlaka waliyonayo tu bali ni pamoja na njia wanazozitumia katika kuzungumza nao.

Kauli za hivi karibuni za Mwenyekiti wa UWT, Mary Chatanda, zimezua mjadala mpana kuhusu kiwango cha ustaarabu katika siasa za nchi yetu.

Nikitafakari naona kuwa haijalishi utofauti uliopo kisiasa, bado taifa linahitaji kuwa na viongozi wanaotambua kuwa maneno yana uzito mkubwa katika kujenga taswira ya uongozi na afya ya taifa.

Lugha kama aliyoitumia mwenyekiti huyu inayoonyesha vitisho, akitamani kuwa na uwezo wa kumaliza wengine wenye mtazamo tofauti, zinaweza kushangiliwa na wafuasi wake lakini ni shangwe ya muda mfupi ambayo kwa taifa inaacha majeraha kwa wanaosikiliza kwa tafakari.

Nilipomsikiliza Chatanda niliwakumbuka watangulizi wa UWT na hasa Bibi Titi Mohamed na Mama Sophia Kawawa, wanawake hawa wa kizazi chao tunaona walivyokuwa na siasa za kujenga.

Misimamo yao na hata lugha walizotumia kujenga hoja katika masuala magumu ya kitaifa ilikuwa ya heshima, busara na utaifa zaidi.

Walituonyesha uongozi si kutoa sauti tu bali kuinua jamii. Ukifuatilia waliyoyafanya wanawake hawa watangulizi utagundua katika kipindi chao, palikuwa na kutofautiana bali walionyesha kutokusigina utu wa wengine.

Walionyesha wazi mwanasiasa ni mfano wa maadili katika jamii.

Bibi Titi kwa wakati wake alionyesha ujasiri akiwa na ushawishi mkubwa kisiasa hasa katika kipindi cha ukoloni akiweza kuhamasisha watu kwa nguvu iliyotokana na uwezo wa kuvuta watu kwa hoja.

Mama Sophia naye aliweza kusaidia uwepo wa mabadiliko mengi hasa katika uwanja wa sheria na tabia zilizokuwa zikiwabagua wanawake kwa heshima kubwa kwa lugha ya utulivu, mshikamano na kujali watu.

Unaweza kusema hawa walikuwepo wakati wa mfumo wa chama kimoja lakini hata wakati huo kulikuwa na siasa za kupingana ndani ya chama hicho hasa kwenye masuala ya wanawake.

Hawa walitumia maneno kama daraja la kuunganisha taifa na siyo kama silaha ya kuumizana.

Kwa hali tuliyonayo sasa nchi yetu ya Tanzania inahitaji kurudi katika siasa za ustaarabu. Ni vyema viongozi wakatambua kuwa vijana wanajifunza kutoka kwao.

Lugha ya chuki ikitoka kwa kiongozi wa juu tena wa umoja wa wanawake, husambaa chini kwa kasi na huweza kuathiri wengi kwa njia moja au nyingine.

Lugha ya hekima huweza kujenga kizazi chenye uvumilivu, heshima na zaidi uwezo wa kusikilizana hata panapokuwa na utofauti wa kisiasa.

Demokrasia yetu haiwezi kuimarika kwa maneno makali na ya kuvunja utu bali itaimarika ikiwepo nguvu ya hoja inayojengwa na viongozi.

Taifa letu likirudi kwenye misingi iliyojengwa na waasisi kama Mwalimu Julius Nyerere aliyefanya kazi na wamama hawa wa mfano, tutajihakikishia taifa lililo salama zaidi.

Lazima tufahamu kuwa lugha ya viongozi katika ngazi yoyote ni kioo cha ustaarabu wa taifa. Dunia ni kijiji mambo yanasambaa haraka na kufika mbali, viongozi watambue hilo.

Tujue wazi kabisa kwamba taifa litajengwa si kwa nguvu ya sauti za viongozi bali kwa hekima ya kauli zao.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

■ Habari

# Ni Mkina mwandishi bora Tanzania



Na Mwandishi WETU

MWANDISHI wa habari mkongwe nchini na Mhariri Mkuu wa Pambazuko, Simon Martha Mkina, ameibuka kuwa mwandishi bora wa habari nchini kwa mwaka 2025.

Umahiri wa Mkina katika uandishi wa habari umetambuliwa kupitia tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania (EJAT), zinazoandaliwa kila mwaka na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Pamoja na Mkina, mwandishi mwingine mkongwe, Dkt. Maurice Samwilu Mwaffisi naye alitunukiwa tuzo ya Mafanikio ya Maisha katika Uandishi wa Habari (Lifetime Achievement in Journalism Award - LAJA) 2025.

Pia, Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Jamhuri, Jackton Manyerere akiibuka kuwa mhariri bora wa mwaka 2025.

Wakongwe hao watatu wameandika historia mpya baada ya kutwaa tuzo mbili za juu zaidi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2025.

Mashindano hayo ndiyo yenye hadhi kubwa zaidi katika taaluma ya uandishi wa habari nchini.

Historia hii inatokana na ukweli kuwa Mkina, Manyerere na Dkt. Mwaffisi wamekuwa washindi wa kwanza katika tuzo hizo ambazo mchakato wake, tangu waandishi kuwasilisha kazi zao na uchambuzi wa majaji katika kutambua kazi bora, hufanyika kimtandao.

Dkt. Mwaffisi ni mwandishi, mwalimu na kiongozi mwenye uzoefu wa muda mrefu katika tasnia ya habari, alitangazwa mshindi wa tuzo hiyo hutolewa kwa wanahabari waliotoa mchango mkubwa na wa kudumu katika maendeleo ya taaluma, ikiwemo kufundisha waandishi, kuandika vitabu vya taaluma ya habari, kulea waandishi wachanga, kuongoza vyumba vya habari, kutetea uhuru wa vyombo vya habari na kuimarisha misingi ya taaluma nchini.

Katika kinyang'anyiro hicho Mkina aliwabwaga Sanula Athanas wa gazeti la Nipashe na Abdallah Kurwa wa ITV.

Mkina aliibuka Mwandishi Bora wa Mwaka 2025 baada ya kunyakua tuzo nyingine mbili; kwanza alitunukiwa tuzo ya mwandishi wa habari bora ya afya kwa mwaka 2025. Kisha akatunukiwa nyingine ya ubobevu na umahiri wa habari bora ya uchunguzi kwa mwaka 2025.

Mkina amejizolea ushindi huo kutokana na ubora wa kazi zake za uandishi zilizokuwa na athari chanya kwa jamii, kuzingatia viwango vya juu vya taaluma na maadili ya uandishi wa habari, pamoja na kuonyesha ubunifu na mchango wa kipekee katika mwaka 2025.

Inaendelea Uk.13

# Ni Mkina mwandishi

Inatoka Uk. 12

Washindi hao wawili; Mkina na Dkt. Mwaffisi walikabidhiwa hundi za mfano zenye thamani ya shilingi milioni tatu kila mmoja kama sehemu ya kutambua mchango wao katika taaluma ya habari. Pia Mkina alipata shilingi milioni moja nyingine kwa ushindi wa habari zake mbili. Manyerere alipata shilingi milioni moja.

Kilele cha Tuzo za EJAT 2025 kilifanyika Mei 29, 2026, katika ukumbi wa Hoteli ya Four Points by Sheraton (New Africa), jijini Dar es Salaam. Hafla hiyo ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya habari na kurushwa mubashara kupitia Azam TV pamoja na majukwaa mbalimbali ya mitandao ya kijamii.

Mkina ni miongoni mwa waandishi wachache ambao kazi zao zilipenya mchakato mkali wa kuchambua kazi za waandishi ulianza kutumika na MCT mwaka huu.

Ukali wa mchakato huo unatokana na vigezo vya hali ya juu vilivyowekwa ili kushindanisha kazi hizo.

Jambo kubwa ambalo lilizingatiwa katika mchakato huo siyo uandishi tu bali uandishi ambao umeleta mabadiliko chanya katika jamii.

Ni kwa kupitia kigezo hicho kikuu na vigezo vingine, habari iliyochunguzwa na Mkina kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu kuhusu upungufu wa magari ya kubebea wagonjwa nchini, ikakidhi vigezo na kuibuka kuwa habari bora kwa mwaka 2025.

Jumla ya kazi 594 ziliwasilishwa, huku habari moja ya Mkina ikiibuka kidedea.

Kutokana na maombi ya wasomaji wetu wengi, habari iliyoshinda itachapishwa wiki ijayo

### Mkina ashukuru

Katika salamu zake fupi baada ya kutangazwa mshindi, Mkina aliwashukuru wazazi wake kwa malezi waliyompa pamoja na walimu waliomkuza katika taaluma ya uandishi wa habari.

Aliwashukuru pia wafanyakazi wenzake wa Pambazuko akisema ushindi wake unatokana




na kazi za pamoja na wenzake hao.

Alisema tuzo hiyo ya EJAT ya mfumo mpya wa kidijiti imeamsha ari yake ya kuendelea kufanya kazi za uandishi kwa bidii, weledi na umakini mkubwa ili aweze kutoa mchango wake kikamilifu katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo na wakati huohuo akitumia uwezo wake kufunza vijana wanaochipukia kwenye taaluma.

Mkina hadi sasa amejizolea tuzo 17 za umahiri katika uandishi wa habari za uchunguzi na utawala bora kutoka ndani na nje ya Tanzania.

### Vigezo

Kulikuwa na vigezo vikubwa vinne vya kupima kazi za uchunguzi zenye ubora ambavyo vimeainishwa na MCT; ustadi wa uchunguzi, ushahidi wa matokeo halisi, uwajibikaji na maslahi ya umma pamoja na ufundi na ubunifu katika uandishi na uzalishaji.

Ilielezwa kuwa katika kuchuja kazi hizo, majaji hawakuangalia jina mwandishi, uzoefu wake au chombo anachofanyia kazi bali ubora wa kazi husika.

Pamoja na kupima ubora huo, majaji walikataka kujiridhisha zaidi kuhusiana na matokeo yaliyoletwa na habari husika na hivyo wakafuatilia matokeo halisi yaliyotokana na kuchapishwa kwa habari hizo.

Inaendelea Uk.14

## Habari

Simon Martha Mkina akipokea cheti na hundi kutoka kwa mwakilishi mkazi wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID) Tanzania mwaka 2008 baada ya kuchaguliwa kuwa mwandishi bora wa mwaka huo – ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika nchini. Katikati ni mfanyabiashara Reginald Mengi, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye hafla iliyofanyika Dar es Salaam. (Picha kutoka maktaba ya Pambazuko).




# Ni Mkina mwandishi

Inatoka Uk. 13

Chini ya vigezo hivyo, habari ya Mkina ikabainika kuleta matokeo makubwa chanya kwani pamoja na mambo mengine habari hiyo iliisukuma Wizara ya Afya kuongeza bajeti ya ununuzi wa magari ya wagonjwa na ujenzi wa vituo vya huduma za dharura katika hospitali nyingi nchini kwa mwaka ujao wa fedha.

Bajeti hiyo tayari imeshawasilishwa bungeni na kupitishwa na kinachosubiriwa sasa ni utekelezaji wake.

Mkina ameahidi kuendelea kulifuatilia suala hilo kuona iwapo kweli wizara itatekeleza ahadi hiyo.

"Ni lazima nifuatilie suala hili hadi mwisho kwa sababu ni suala linalohusu maisha ya watu. Wapo watu wamepoteza maisha kwa sababu tu hakukuwepo gari la wagonjwa la kuwakimbiza hospitali au gari lililokuwepo halikuweza kufanya kazi kwa sababu ni bovu au lilikosa mafuta," anasema Mkina alipoongea na Pambazuko.

### Kauli ya majaji

Kiongozi wa jopo la Majaji wa MCT walioopitia kazi hizo, Jesse Kwayu, alisema kuwa mchakato huo mpya wa kuchuja ubora wa habari uliowekwa na MCT, pamoja na vigezo vilivyoboreshwa, umefanikisha kuzipata kazi ambazo ni mahiri katika uandishi wa habari.

Jesse alisema mfumo huo mpya uliwawezesha majaji kufanya kazi kila mmoja akiwa kwake bila ya kuhitaji kukusanyika pamoja.

Alisema hakukuwa na jaji ambaye aliona kazi ya jaji mwingine kwani kila mmoja alifanya kazi kwenye mfumo kwa kuangalia kazi zake tu.

Akabainisha kuwa mfumo huo una usiri mkubwa na hivyo kuondoa uwezekano wa kula njama za upendeleo.

Alisema mfumo huo mpya uliwawezesha majaji kufanya kazi bila ya mahitaji ya kuweka kambi.

"Yupo jaji ambaye aliweza kukamilisha kazi zake akiwa nje ya bara la Afrika," alisema na kuongeza: "Tumebaini kuwa matumizi ya mfumo huu yamewezesha pia kupunguza gharama za uendeshaji."

Alisema ni kwa kupitia vigezo hivyo na mchakato jopo alilolíongoza limebaini, kwa masikitiko, kuwa uandishi wa habari za uchunguzi nchini unapitia katika changamoto kubwa.

Aidha, alisema, mfumo umeonesha pia kuwa vyombo vya habari vya mtandaoni vimeanza kufuata weledi wa uandishi wa habari na hivyo kuongeza wigo wa jamii kupata habari za uhakika.


Ernest Sungura

# Jaji Kayobera, Sungura

Inatoka Uk. 4

Aliwataka waandishi wa habari vijana kuendelea kulinda misingi ya taaluma hiyo na kutunza heshima ya vyombo vya habari vilivyojengwa kwa juhudi za watangulizi wao.

**Kauli ya MCT**

Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura, alielezea dhamira ya MCT kuendeleza tuzo hizo akisema maboresho yaliyofanyika kuingiza teknolojia kwenye mchakato wa kutafuta waandishi mahiri ni moja ya vielelezo vya dhamira hiyo.

Alisema kauli mbiu ya EJAT mwaka huu ya kusherehekea uandishi wa habari nwenye tija inakumbusha kwamba umahiri wa kweli hupimwa kwa tija inayoletwa kwa jamii kupitia taaluma.

Sungura alisema sherehe hizo za 16 za EJAT ni fursa ya kutafakari kuhusu tasnia ya habari na utangazaji nchini.

"Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuwa waandishi wa habari nchini bado wanakabiliwa na ajira zisizo na uhakika, wanapitia vitisho na changamoto za kidijitali,"alisema.

Akabainisha kuwa kutokana na changamoto hizi waandishi na vyombo vya habari vimeshindwa kutekeleza wajibu wao sawa sawa na kuifanya jamii kujiuliza maswali iwapo vyombo hivyo vipo kwa ajili yao.

"Lakini katikati ya changamoto hizi wapo waandishi wa habari mahiri ambao waliamua kuibua simulizi zinazotupatia nguvu na uhalali wa kukutana hapa kufurahia matunda ya uandishi wa habari wenye tija kwenye taifa letu," alisema.

Sungura alisema waandishi hao hawakukatishwa tamaa na changamoto hizo na wakaendelea kupaza sauti za wananchi na kugusa maisha ya watu na kuweka ukweli hadharani.

Alisema ingawa wengi hawakufikia hatua ya kazi zao kutambuliwa katika ngazi hiyo, lakini EJAT ya mwaka huu inapaswa kuwa chachu kwa waandishi wengine kuboresha kazi zao ili nao watekeleze kwa vitendo dhima ya vyombo vya habari nchini.

Akielezea mabadiliko yaliyofanyika katika mchakato wa EJAT, Sungura alisema tuzo za mwaka huu zimekwenda mbali zaidi ya kuangalia ubora wa kazi zilizochapishwa au kutangazwa.

"Tunahoji maswali kama habari hii ina umuhimu kwa jamii inayohusika? Je imegusa vipi maisha ya watu katika jamii hiyo? Inachochea uwajibikaji? Je imeandaliwa kwa weledi?" alisema.

Sungura alisema kuwa uandishi wa habari wa tija unaonesha kuwa kushika kalamu au kamera mikononi mwao ni sawa na kushika mustakabali wa taifa.

Alisema ipo haja kwa wadau wa habari kushikamana na kuhakikisha kuwa waandishi wa habari hawatumiki kwa maslahi ya wanasiasa au wafanyabiashara kwani kufanya hivyo kutaondoa kabisa dhima yao kwa jamii.

"Mwito wangu kwa wahariri ni kuwa wasikubali kutumiwa au kununuliwa na wanasiasa na wenye fedha wachache, ni hatari kwa taifa,"alisisitiza.

Rais wa MCT, Jaji (mstaafu) Bernard Luanda, alisema inatia moyo kuona kuwa licha ya changamoto lukuki zinazovikabili vyombo vya habari nchini, mabadiliko chanya yameanza kuonekana kutokana na juhudi za pamoja na kukabiliana na changamoto hizo.

Pia aliisifu serikali kwa kuchukua hatua za kuondoa baadhi ya vikwazo na changamoto hizo kama vile mabadiliko ya kanuni za maudhui mitandaoni.

Akitoa mfano alibainisha mathalani kuwa kupitia marekebisho yaliyofanywa na serikali, ada ya mtu kusajili chombo cha habari mtandaoni imepunguzwa na hivyo kuwawezesha watu wengi kuimudu.

Aidha, alisema utaratibu ulioanzishwa hivi karibuni wa kutoa mikopo kwa watengeneza maudhui mitandaoni kumefungua milango kwao.

Habari

# Mzee adai mtoto wake kamtupa porini




Na Mwandishi WETU

VITENDO vya ukatili kwa wazee vimeendelea kushamiri baada ya kijana mmoja kudaiwa kumtesa baba yake na kisha "kumtupa" porini.

Tukio hilo la kusikitisha na kushangaza limetokea jijini Dar es Salaam katika eneo la Mbezi.

Damas Christian mwenye umri wa miaka 63, anaelezwa kutupwa porini katika eneo la Masaki, Mbezi kwa Msuguri akiwa na makovu mwilini yanayoashiria kuwa alikuwa akipata kipigo.

Mzee huyo alionekana kudhoofu kiasi kwamba mtu wa kwanza kumuona alidhani amefariki dunia, hata hivyo, baada ya kuita umati kumchunguza kwa karibu, ikabainika kuwa mzee huyo alikuwa bado hai.

Umati uliamua kumchukua na kumpeleka hospitali kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Akisimulia mkasa huo, mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Christina Herman, ambaye ni mmiliki wa eneo ambalo mzee huyo alikuwa ametupwa, alisema mzee Christian alikutwa majira ya saa 12 alfajiri ya Mei 27 mwaka huu akiwa hajitambui.

Alikutwa akiwa amevaa nguo zilizochoka na kutapakaa kinyesi.

"Majira hayo tulianza kusikia mbwa wakibweka mfululizo ila awali hatukujua kilichokuwa kinaendelea kutokana na eneo hilo kuwa na pori lenye majani mengi…"

"Ilipofika alfajiri majira ya saa 12 kuna wapita njia waligundua kuwepo kwa mtu akiwa amelala na kuonekana ameshambuliwa na kutelekezwa ndani ya eneo langu..."

"Niliitwa na mpita njia mmoja na kwenda kumuona mzee huyo na kubaini kuwa mtu huyo ambaye namfahamu alikuwa hai, nilichukua hatua ya kumpigia mjumbe wa nyumba kumi, Salum Bwenzi, ambaye alisaidia kumpata mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, ambaye alitushauri apelekwe Hospitali ya Kimara, tulimpeleka na kupokelewa na kuanza vipimo mbalimbali," anasema Christina.

Anasema vipimo hivyo vilionesha kuwa mzee huyo hakuwa anasumbuliwa na ugonjwa wowote, bali kudhoofu kwake kulitokana na njaa ikimaanisha kuwa hajala chakula kwa muda mrefu.

"Daktari alitushauri tumrudishe nyumbuni lakini tuanze kumpatia uji na vyakula laini vya maji maji kama mtori na viazi,"anasimulia.

Akizungumza na Pambazuko, Christina anasema aliwahi kuishi na mzee huyo baada ya kwenda kuomba hifadhi kwake, akieleza kuwa alikuwa mhitaji, lakini baadaye alipatikana mtu aliyeeleza kuwa ni baba yake.

Mtu huyo, akiwa wa makamo ya miaka kati ya 40 na 50, alijitambulisha kuwa anaitwa Ignas Damas. Alimchukua Septemba 2025.

Christina anasema aliishi na mzee huyo kwa miaka 24 akimtunza kama mhitaji kwa kushirikiana na waumini wa Jumuia ya Mtakatifu Kizito na Mtakatifu Emmanuel na vyama ya Kitume vilivyopo chini ya Kanisa Katoliki katika Parokia ya Temboni, Dar es Salaam.

Inaendelea Uk.17

# Mzee adai mtoto...

Inatoka Uk. 16

"Mzee huyu ambaye tulizoea kumuita "Babu", tulikuwa tukimtunza vizuri sana kwa sababu alidai hakuwa na ndugu wala jamaa, sisi tuliamua kumtunza hadi pale alipojitokeza huyo kijana na kusema huyo baba yake.

"Hivyo tukamwachia amchukue aende kumtunza, alitoka kwangu akiwa na afya njema, lakini baada ya hapo hutukuwa na mawasiliano naye hadi alipokutwa akiwa hivi," alisema.

Akizungumza na Pambazuko kwa taabu huku akibubujikwa machozi, Mzee Christian anadai usiku huo wa Mei 27 aliletwa na mwanaye Ignas na kumtupa eneo hilo bila msaada wowote.

"Tangu anichukue hapa mwaka jana mwanangu alikuwa ananipiga na kuninyima chakula…"

"Muda mwingi sikuwa hata napata muda wa kuoga, nimeishi kwa mateso ya manyanyaso, alifikia hatua ya kuchoma moto sehemu ya mguu wangu wa kulia," anasema huku akionyesha kidonda kwenye mguu huo.

Kutokana na hali ya mzee huyo, Mwenyekiti wa Kanda ya Mtakatifu Magdalena, Thomas Ndenzako, ameiomba serikali kumsaidia kwa kumpatia hifadhi na huduma nyingine kwa kuwa hajiwezi kwa kila kitu.

Pambazuko lilimpata Ignas ambaye alisema kwa kifupi kwamba hajawahi kumpiga wala kumnyanyasa baba yake.

Ignas alisema alichofanya ni kumpeleka baba yake kwenye nyumba ya Christina ambako ndiko alimfahamu kwa mara ya kwanza kwani hakuwahi kutambulishwa kwa baba yake tangu kuzaliwa hadi alipokuwa mtu mzima.

Ignas anadai kwamba yeye hajamtelekeza mzazi wake huyo bali alimrudisha hapo alipomkuta akiishi awali.

Amelieleza Pambazuko kuwa alimrudisha hapo kwa Christina kwa kuwa alikuwa na safari ya kwenda Arusha na kwenye chumba chake hakukuwa na mtu wa kumhudumia.

Akizungumza kutokea Arusha, Ignas anaeleza kuwa majeraha aliyonayo mzee wake yalitokana na kuumia kwa sababu aliteleza kwenye ngazi wakati anapanda hapo kwenye chumba chake.




*Mwenyekiti wa Kanda ya Mtakatifu Magdalena, Thomas Ndenzako (kulia) akishiriana na Mwenyekiti wa Jumuia ya Mtakatifu, Emmanuel Archard Muchunguzi (wa pili kushoto) kumhudumia Mzee Damas Christian ambaye alidai kutupwa na kutelekezwa na mtoto wake katika eneo la Masaki Mbezi kwa Msuguli, Jijini Dar es Salaam mwishoni mwa Wiki. (Na Mpigapicha Wetu)*

# Tanzania yaunga mkono ubunifu mpya sekta ya fedha


Dkt. Natu Mwamba

Na Benny MWAIPAJA, Brazzaville

TANZANIA imeelezea msimamo wake wa kuunga mkono mbinu za fedha za mseto zitakazosaidia kuimarisha sekta za usafiri wa anga na afya Afrika, ikieleza kwamba hakuna chanzo kimoja kitakachoweza kuziba upungufu wa miundombinu ya bara hilo.

Akizungumza akiwa Gavana Mbadala wa Tanzania kwenye mkutano ulioandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kuhusu mifumo mipya ya kifedha inayolenga kupunguza vihatarishi katika sekta kadhaa ikiwemo ya anga na afya, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba alisema Tanzania haina tatizo na mifumo hiyo.

Alisema mifumo hiyo itasaidia sana kwani inatoa suluhisho la vitendo, nafuu na linaloendana na vipaumbele vya kitaifa vya Tanzania.

"Tunasisitiza matumizi ya rasilimali za umma na binafsi pamoja na dhamana na msaada kutoka kwa washirika. Hatuwezi kutegemea chanzo kimoja pekee," alisema Dkt. Mwamba, akiongeza kuwa ni muhimu kuzingatia udhibiti wa deni linalozidi kukua katika nchi za Afrika.

Alisisitiza kuwa usafiri wa anga ni kichocheo cha biashara, utalii, uwekezaji na ukuaji wa kikanda na kwamba Tanzania inakaribisha uwekezaji wa ubunifu kwa ajili ya uboreshaji wa viwanja vya ndege, uimarishaji wa usalama, utengenezaji wa mifumo ya usafirishaji na kuunganisha safari za kikanda kwa ufanisi. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kituo cha usafiri kwa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Vilevile, kuhusu huduma za afya, Dkt. Mwamba alibainisha kuwa mifumo thabiti ya afya ni nguzo ya uzalishaji, rasilimali watu na ustahimilivu wa kiuchumi inayohitaji fedha za kuaminika na nafuu kwa ajili ya dawa muhimu, vifaa vya kisasa na miundombinu ya afya inayoweza kustahimili mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Dkt. Mwamba alieleza mahitaji ya Tanzania kwa AfDB kuwa ni pamoja na kuendeleza msaada kwa ajili ya maandalizi ya miradi ili kuibua miradi inayoweza kuvutia wawekezaji, hususan kutoka sekta binafsi, upatikanaji wa dhamana na kuwa na masharti nafuu zaidi ya mikopo kutoka Taasisi za Fedha, ikiwemo AfDB.

"Tanzania iko tayari kushirikiana na AfDB na wadau wote kwa uwekezaji wa matokeo dhahiri kwa wananchi wetu," alisema Gavana Mbadala huyo.

Mkutano huo uliofunguliwa na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Sidi Ould Tah, uliwaleta pamoja wadau wa maendeleo, mawaziri wa fedha, magavana wa benki kuu, wawekezaji na viongozi wa serikali kuzungumza kuhusu njia za kuondoa vikwazo vinavyoweka hatari kwa wawekezaji na kuleta mbinu za upatikanaji wa fedha zenye tija kwa miradi ya usafiri na afya Afrika.

# Ndoto ya maendeleo, mtihani wa mageuzi Tanzania



Na Steven MMBOGO

KATIKA kipindi cha miongo kadhaa baada ya uhuru, Tanzania imeendelea kutafuta njia sahihi ya kujenga uchumi imara, jumuishi na unaoweza kujitegemea.

Kutoka katika falsafa ya ujamaa na kujitegemea chini ya Mwalimu Julius Nyerere, hadi sera za soko huria zilizoanza kushika kasi miaka ya 1990, Tanzania imekuwa katika safari ya kutafuta usawa kati ya maendeleo ya kiuchumi, ustawi wa wananchi na uhuru wa kisera.

Leo, mjadala kuhusu mwelekeo wa uchumi wa Tanzania umechukua sura mpya, ukiangazia viwanda, nishati, uwekezaji, deni la taifa, ajira kwa vijana na usimamizi wa rasilimali za taifa.

Katika mazingira ya ushindani wa kimataifa, Tanzania haiwezi tena kutegemea uchumi wa malighafi pekee. Hili limeifanya ajenda ya viwanda kuwa mhimili muhimu wa sera za maendeleo.

Msukumo wa kuwa na viwanda vingi siyo tu suala la kujenga majengo ya viwanda, bali ni mchakato wa kubadilisha muundo mzima wa uchumi kutoka utegemezi wa bidhaa ghafi kwenda uzalishaji wenye thamani kubwa zaidi.

Taifa lenye viwanda imara huongeza ajira, huimarisha mapato ya serikali na hupunguza utegemezi wa bidhaa kutoka nje. Hata hivyo, changamoto bado ipo katika kuhakikisha kuwa viwanda hivyo vinaunganishwa na uzalishaji wa ndani, teknolojia, utafiti na nguvu kazi yenye ujuzi.

Katika msingi huo, sekta ya nishati imekuwa mhimili wa mustakabali wa uchumi wa Tanzania. Hakuna uchumi wa kisasa unaoweza kukua bila nishati ya uhakika, nafuu na endelevu. Uwekezaji katika miradi ya umeme, gesi asilia na nishati mbadala unapaswa kuonekana si kama miradi ya kisiasa bali kama uwekezaji wa kimkakati kwa vizazi vijavyo.

Uchumi wa nishati unahitaji uwazi, ushindani wa haki na sera zinazovutia ubunifu wa kiteknolojia.

Bila hayo, gharama za uzalishaji hubaki juu, viwanda hukosa ushindani na wananchi huendelea kubeba mzigo wa maisha magumu.

Sambamba na hilo, siasa za miundombinu zimeendelea kuwa sehemu muhimu ya mjadala wa maendeleo. Ujenzi wa reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege umepewa nafasi kubwa katika simulizi ya maendeleo ya taifa. Kwa kiwango fulani, uwekezaji huu umeongeza muunganiko wa kiuchumi na kurahisisha biashara.

Hata hivyo, swali muhimu linabaki: je, miradi hii inajengwa kwa misingi ya tija ya kiuchumi au kwa mantiki ya kisiasa? Miundombinu yenye manufaa lazima iweze kuchochea uzalishaji, biashara na ajira, siyo miradi yenye sifa tu, inazobeba hadhi ya kisiasa bila kuleta faida pana kwa wananchi.

Katika hatua hiyo ndipo dhana ya utaifa wa kiuchumi (economic nationalism) inapojitokeza kwa nguvu. Mataifa mengi duniani yameanza kurejea katika sera zinazolinda maslahi ya ndani dhidi ya utegemezi mkubwa wa nje.

Inaendelea Uk.22



# Ukatili wa IGP Mahita gumzo

Na Mwandishi WETU

BAADHI ya watu wamemtaka aliyekuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Omari Mahita kuomba radhi Watanzania kutokana na ukatili aliowafanyia wakati akiwa madarakani.

Hivi karibuni Mahita akiliri kuwa alikuwa katili katika uongozi wake.

“Ni kweli kabisa, tena katili vibaya sana tena usicheze na mimi, nilikuwa katili, katili kweli,”alisema IGP huyo wa zamani wakati akijibu swali katika kipindi cha MS Podicast.

Mahita alikuwa IGP Polisi kuanzia mwaka 1995 hadi 2006.

Mahita ametoa kauli hiyo na kuibua hisia katika kipindi ambacho masuala ya wananchi kuumizwa na Jeshi la Polisi yakiwa yameshamiri.

Kauli yake imeibua ukosoaji huku baadhi ya watu wakaiita kama kielelezo cha malalamiko dhidi ya jeshi hilo nchini, hasa wakati ambao taifa linatafuta majibu ya matukio ya mauaji yaliyotokea Oktoba 29, 2025.

Baadhi walisema kauli hiyo ya Mahita inathibitisha madai ya muda mrefu ya vitendo vya ukatili na unyanyasaji unaofanywa na askari polisi dhidi ya raia yaliyokuwa yakitolewa hasa na vyama vya upinzani wakati Mahita alipokuwa akiongoza chombo hicho cha dola.

Inaendelea Uk.21

# Ukatili wa Mahita

Inatoka Uk. 20

Akizungumzia kuhusu mauaji ya Oktoba 29, 2025, Mahita alielezea jinsi mabadiliko ya kitamaduni na kuporomoka kwa heshima ya jadi kulivyovuruga.

Lakini akazitetea mamlaka za serikali akisema zilionyesha uvumilivu wa hali ya juu katika kipindi hicho kwa kukataa kuingizwa katika mtego wa mapambano ya ghasia, jambo ambalo lililinda na kuhifadhi utulivu wa kitaifa.

"Ili kuepuka hatari ya kuiga mapinduzi au maandamano ya nchi za nje, kuna ulazima wa kulinda amani ya ndani kupitia busara za ndani ya nchi badala ya ushawishi kutoka nje,"amesema Mahita.

Akizungumzia kuhusu madai ya Jeshi la Polisi kuingiliwa na wanasiasa, Mahita alikiri kuwa ni kweli hivi sasa jeshi hilo linaingiliwa na wanasiasa.

"Miongoni mwa mambo niliyopambana nayo ni kuzuia wanasiasa kuingilia Jeshi la Polisi na walikuwa wakijaribu kutoa maelekezo hasa ya watu kukamatwa nilikataa mapema," amesema.

IGP huyo mstaafu amesema katika uongozi wake hakuwa akipokea amri ya kukamata mtu kutoka kwa kiongozi mwingine yeyote isipokuwa rais, makamu wa rais na waziri mkuu.

Katika hilo alisisitiza kuwa waziri au viongozi wengine hawana mamlaka ya kuamrisha askari kukamata mtu.



Kuhusu matukio ya utekaji na watu kupotea, IGP mstaafu Mahita alisema wakati wa uongozi wake hakukuwa na matukio ya aina hiyo.

"Mtu anapoteaje?... Wakati ule mtu akipotea ilikuwa rahisi kujua alikopotelea, tofuati na sasa ambapo ambayo system imekuwa kama ugonjwa wa ukoma," amesema Mahita.

Mahita alishangaa kuwa watu wanapotea lakini mamlaka za uchunguzi na upelelezi hazifahamu yanayotokea.

**Asichokisahau**

Alipoulizwa ni tukio gani ambalo hatalisahau katika uongozi wake wa miaka 10, Mahita alisema mauaji ya watu huko kisiwani Pemba mwaka 2001 ni tukio ambalo siku zote litabaki katika kumbukumbu zake.

Tukio hilo, lililotokana na CUF kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu lilisababisha vifo vya watu takribani 21, majeruhi wengi na wengine kukimbilia nchi jirani ya Kenya ili kuokoa maisha yao.

Tukio hilo lilitokana na mgogoro mkubwa wa kisiasa uliosababisha wananchama wa CUF kuandamana kupinga matokeo ya uchaguzi.

Katika matokeo hayo, Dkt. Amani Abeid Karume wa CCM alitangazwa kuwa mshindi wa urais wa Zanzibar akifuatiwa na mgombea wa CUF, hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Akizungumza katika mahojiano hayo, Mahita alisema hatasahau tukio hilo kwani askari wake walichinjwa.

"Baadaye wakaja wakaelekea kwenye kituo cha polisi… pale sisi tulidhibiti na walikufa hilo ndilo tukio kubwa sana.

"Hii ndio wengi walikimbilia shimoni nilipeleka helkopta ikawa inazunguka kule kule, basi wakawa wananiita mtwana huyo…. huyo Mahita mtwana anaua watu… kwa kweli Maalim Seif, Mungu amlaze salama peponi.

"Tukio lile hakika sitalisahau, mpaka leo Wapemba hawalisahau ikifika tarehe hiyo wanalikumbuka sana," amesema Mahita.

Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamini Mkapa naye aliwahi kukiri katika kitabu chake cha Maisha Yangu, Kusudio Langu, kuwa mauaji hayo ya Pemba ni kati ya tukio lililotia doa uongozi wake wa miaka 10.

Biashara

# Ndoto ya maendeleo

Inatoka Uk. 19

Kwa Tanzania, utaifa wa kiuchumi unapaswa kumaanisha kulinda rasilimali za taifa, kukuza uzalishaji wa ndani na kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika kwanza na uchumi wao.

Hata hivyo, utaifa wa kiuchumi usipotekelezwa kwa busara unaweza kugeuka kuwa mazingira yasiyotabirika kwa wawekezaji. Hivyo, changamoto kubwa ni kujenga usawa kati ya kulinda maslahi ya taifa na kudumisha mazingira rafiki kwa biashara na uwekezaji.

Kwa upande wa mazingira ya uwekezaji, Tanzania imeendelea kuwa na nafasi ya kuvutia kutokana na rasilimali zake, jiografia yake na soko linalokua.

Lakini wawekezaji wa ndani na wa nje huhitaji zaidi ya kauli za kisera; wanahitaji uhakika wa sheria, taasisi zinazotabirika na mfumo wa haki usio na upendeleo. Pale ambapo sera hubadilika ghafla au maamuzi ya kiuchumi yanaonekana kuongozwa zaidi na matakwa ya kisiasa kuliko kanuni za uchumi, imani ya wawekezaji hupungua.

Uchumi wa kisasa hujengwa juu ya taasisi imara, si juu ya matamko pekee.

Hili linaenda sambamba na nafasi ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI). Uwekezaji wa kigeni unaweza kuleta mtaji, teknolojia na ajira.

Lakini pia unaweza kuwa chanzo cha utegemezi ikiwa taifa halitaweka mikakati ya kuhakikisha uhamishaji wa maarifa, ushiriki wa wazawa na manufaa ya muda mrefu kwa uchumi wa ndani.

Tanzania inapaswa kuwa na uwezo wa kujadiliana kwa kujiamini na wawekezaji wa kimataifa bila kuonekana kama taifa linalouza rasilimali zake kwa gharama ndogo ili tu kupata mtaji wa haraka.

Kadri taifa linavyoendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, mjadala kuhusu deni la taifa umeendelea kuongezeka. Kukopa siyo kosa katika uchumi wa kisasa; tatizo hutokea pale mikopo inapokuwa mikubwa kuliko uwezo wa uzalishaji wa taifa.

Deni linakuwa na maana ikiwa fedha zinazokopwa zinawekeza katika miradi inayoongeza tija ya uchumi na mapato ya baadaye. Lakini pale mikopo inapogeuzwa kuwa mzigo wa matumizi yasiyo na tija, taifa hujikuta likiingia katika mzunguko wa utegemezi wa kifedha na kupunguza uwezo wake wa kupanga sera kwa uhuru.

Aidha, usimamizi wa rasilimali za taifa umeendelea kuwa kipimo muhimu cha uadilifu wa mfumo wa uchumi. Tanzania imebarikiwa kuwa na madini, gesi, ardhi, misitu na bahari.

Lakini historia ya mataifa mengi yenye rasilimali nyingi inaonyesha kuwa utajiri wa asili pekee hauhakikishi maendeleo. Kinachohitajika ni uwazi, uwajibikaji na mikataba yenye maslahi ya taifa. Bila hayo, rasilimali zinaweza kuwa chanzo cha migogoro, ufisadi na ukosefu wa usawa wa kiuchumi.

Katika mazingira hayo yote, sekta isiyo rasmi imeendelea kuwa uti wa mgongo wa maisha ya wananchi wengi. Mamilioni ya Watanzania wanajipatia kipato kupitia biashara ndogo ndogo, usafirishaji, kilimo cha kujikimu na shughuli nyingine zisizo rasmi.

Hata hivyo, sekta hii mara nyingi huonekana kama eneo la kukusanya kodi badala ya kupewa mazingira ya kukua. Uchumi jumuishi unapaswa kuangalia namna ya kuhamisha shughuli hizi kutoka hali ya "survival economy"kwenda uchumi wenye tija, mitaji na ulinzi wa kijamii.

Hakuna mjadala wa uchumi wa Tanzania unaoweza kukamilika bila kugusia tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana. Kila mwaka maelfu ya vijana wanaingia kwenye soko la ajira huku uchumi ukishindwa kuzalisha nafasi za kutosha.

Hii si changamoto ya kiuchumi pekee bali pia ni changamoto ya kijamii na kisiasa.

Taifa lenye vijana wengi wasiokuwa na matumaini ya kiuchumi hujenga mazingira ya kukata tamaa, ongezeko la uhalifu na kupungua kwa imani kwa taasisi za dola.

Suluhisho la kweli haliwezi kuwa ajira za muda mfupi au ahadi za kisiasa, bali ni mageuzi ya elimu, ubunifu, uwekezaji katika teknolojia na uchumi unaochochea uzalishaji.

Mwisho wa yote, mwelekeo wa uchumi wa Tanzania hautaamuliwa na ukubwa wa miradi pekee, bali na uwezo wa taifa kujenga uchumi unaogusa maisha ya wananchi wa kawaida. Maendeleo ya kweli hayaonekani tu katika takwimu za ukuaji wa uchumi, bali katika ubora wa maisha ya watu.

***Mwandishi wa makala haya ni mchambuzi na mtafiti wa mambo ya jamii na uchumi.***

# Wizara yakwepa hoja ya vikwazo vya Marekani

**Na Mwandishi WETU, DODOMA**

UWEZEKANO wa nchi kuwekewa vikwazo vya kiulinzi na kiuchumi na Marekani limeonekana siyo suala linaloisumbua sana Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Inaonekana kuwa suala hilo haliiumizi kichwa wizara hiyo kwani katika hotuba yake ya Bajeti kwa mwaka 2026/27 haikulizungumzia kabisa.

Kwa kawaida, kupitia hotuba ya Bajeti wizara huzungumzia masuala yote ya msingi ambayo imepanga kuyatekeleza katika mwaka ujao wa fedha.

Lakini katika hotuba yake aliyoiwasilisha bungeni wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dkt. Mahmoud Thabit Kombo, hakuliweka kabisa suala hilo ambalo katika siku za hivi karibuni limezua gumzo kubwa nchini.

Hata Kamati ya Mambo ya Nje ya Bunge katika taarifa yake nayo haikuzungumza chochote kuhusiana na suala hilo ambalo linatishia ustawi wa nchi na wananchi wake iwapo Marekani itatunga sheria hiyo ya kuiwekeza vikwazo Tanzania.

Lakini kutokana na umuhimu wa suala hilo, licha ya kutokuwemo kwenye hotuba ya bajeti, wabunge kadhaa walilijadili suala hilo, tena kwa hisia kali.

Baadhi yao waliionya serikali kuwa inapaswa kuwa makini na suala hilo ili kuhakikisha kuwa Tanzania haifikii hatua ya kuwekewa vikwazo hivyo kwani vitaiumiza nchi.

Wengine wakawalaumu Maseneta hao wawili wa Marekani ambao ndio waliowasilisha muswada unaolenga kutunga sheria itakayoweka vikwazo kwa Tanzania, wakiwatuhumu kuwa wametoa hoja zisizo na ukweli kuhusu Tanzania.



*Dkt. Mahmoud Thabit Kombo*

Suala hilo pia limezua mijadala mizito katika maeneo mengine nchini huku baadhi ya watu wakijitokeza kutoa maoni yao.

Kutokana na mjadala huo mkali bungeni, Waziri Dkt. Kombo alilazimika kulisemea suala hilo wakati akihitimisha majadiliano hayo.

Wabunge waibua hoja

Wa kwanza kuliibua suala hilo bungeni ni Mbunge wa Viti Maalum, Mariamu Mungula, ambaye alisema katika mchango wake kuwa ameuona muswada ambao umewasilishwa katika Seneti ya Marekani na Maseneta wawili ukilenga kutunga sheria inayoitaka serikali ya nchi hiyo kubwa kuiwekeza vikwazo Tanzania.

Akasema muswada huo uliwasilishwa na maseneta kutoka vyama viwili hasimu nchini humo ambao wanaitaka serikali yao kuiwekea vikwazo Tanzania wakiituhumu kwa unyanyasaji wa kisiasa na kidini.

"Huu muswada sasa hivi upo kwenye hatua ya kujadiliwa kwenye kamati yao ya Mambo ya Nje. Hawa ni viongozi wawili vya vyama vya Republican na Democrat na muswada huu si nzuri kwa serikali yetu, kwa hiyo tuuchukulie kwa umakini na umuhimu wake,"alisema mbunge huyo kwa utulivu.

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# PR ni sauti inayolinda heshima ya taasisi, kampuni




KATIKA dunia ya sasa, kampuni au taasisi haiwezi kuishi kwa bidhaa, huduma, mamlaka au majengo pekee. Inaishi kwa imani ya watu.

Imani hiyo ndiyo mtaji mkubwa kuliko fedha, magari, ofisi na matangazo. Ndiyo maana Uhusiano na Umma, maarufu kama PR, siyo kazi ya pembeni tena; ni moyo wa taasisi inayotaka kueleweka, kuaminika na kudumu.

PR siyo kutuma taarifa kwa vyombo vya habari pekee, wala siyo kupiga picha za viongozi wakitabasamu.

Ni taaluma ya kujenga, kulinda na kuendeleza uhusiano kati ya taasisi na jamii inayoizunguka.

Public Relations Society of America inaieleza PR kama mchakato wa kimkakati wa mawasiliano unaojenga mahusiano yenye manufaa kati ya taasisi na umma wake. Hii ina maana kwamba PR bora haizungumzi tu; husikiliza, huchambua, huelewa hisia za wadau na kuishauri taasisi ichukue hatua sahihi.

Kwa kampuni, PR ndiyo ngao ya sifa. Kampuni inaweza kuwa na bidhaa nzuri, lakini kama wateja hawaamini dhamira yake, soko litayumba. Inaweza kuwa na mtaji mkubwa, lakini kama jamii inaiona kama mnyonyaji, heshima itapotea.

Chartered Institute of Public Relations inasema PR ni kuhusu sifa; matokeo ya kile unachofanya, unachosema na kile wengine wanasema kuhusu wewe. Hii ni nukuu yenye somo kubwa; sifa haijengwi na maneno matamu pekee, bali na tabia ya taasisi.

Arthur W. Page, mmoja wa magwiji wa PR ya kisasa, alitoa kanuni ambazo kila taasisi inapaswa kuziandika ukutani: “Sema ukweli,” “thibitisha kwa vitendo,” na “sikiliza wadau.” Hizi ni nguzo tatu za PR yenye uhai. Taasisi inayosema ukweli hujenga uaminifu. Inayothibitisha kwa vitendo hupata heshima. Inayosikiliza wadau huepuka migogoro isiyo ya lazima.

Edward Bernays, anayejulikana kama mmoja wa waanzilishi wa PR ya kisasa, aliiona PR kama taaluma ya kushawishi na kujenga uelewa wa umma.

Lakini katika zama hizi, ushawishi bila ukweli ni hatari. PR ya kisasa haiwezi kuwa pazia la kuficha makosa. Inapaswa kuwa kioo kinachoionyesha taasisi ilivyo, na dira inayoisaidia kuwa bora zaidi.

Kwa taasisi za umma, PR ni daraja kati ya sera na wananchi. Serikali inaweza kuwa na miradi mikubwa, lakini kama wananchi hawaelezwi vizuri, miradi hiyo hukosa umiliki wa jamii.

Kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, PR husaidia kuonyesha thamani ya kazi zao na kuimarisha imani ya wafadhili na wanufaika. Kwa kampuni binafsi, PR hujenga uaminifu wa wateja, wawekezaji, wafanyakazi na jamii.

Ndiyo maana taasisi inayodharau PR inatembea gizani. Haina masikio ya kusikia jamii, haina macho ya kuona hatari ya sifa, na haina sauti ya kueleza dhamira yake.

PR makini siyo mawasiliano mepesi pekee, ni uwekezaji katika heshima, uaminifu na uhai wa taasisi.

***Mwandishi wa safu hii ni Mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***



Na Emmanuel JACOB

# Umuhimu wa mazoezi kukabiliana na msongo



KWA sasa, msongo wa mawazo (stress) umekuwa kama kivuli kinachomfuata kila mtu.

Asubuhi hadi jioni akili zetu zinakabiliwa na shinikizo la maisha, changamoto za kiuchumi, na majukumu ya kifamilia.

Matokeo yake, miili yetu inabaki kwenye hali ya tahadhari kila wakati, jambo hili huathiri mwili na akili.

Katikati ya changamoto hizi, tafiti zinaonyesha umuhimu wa mazoezi katika kukabiliana na msongo wa mawazo.

Watu wengi bado wanaamini kuwa kufanya mazoezi ni kwa ajili ya kupunguza uzito au kujenga misuli pekee. Huu ni mtazamo finyu unaoficha faida kubwa zaidi ya mazoezi.

Pamoja na kujenga mwili, mazoezi ya viungo pia ni tiba ya kisaikolojia na hivyo husaidia kuuweka mwili na akili katika uwiano mzuri.

Unapoanza kukimbia, kucheza muziki, au hata kutembea kwa haraka, unabadilisha mfumo wa ufahamu (ubongo) wako papo hapo.

Mazoezi hufanya kazi kama kifutio cha stress kwa kupunguza uzalishaji wa homoni za cortisol na adrenaline -kemikali zinazosababisha hofu, wasiwasi, na uchovu wa kiakili.

Wakati homoni hizo hasi zikishuka, ubongo wako unaanza kumimina kemikali za furaha zinazojulikana kama endorphins. Kemikali hizi ni kama dawa asili ya kutuliza maumivu na kuleta hisia za amani na furaha ya ndani.

Ndiyo maana baada ya mazoezi makali, hata kama uliingia ukiwa umechoka kiakili, unatoka ukiwa na tabasamu, una nguvu mpya, na mtazamo chanya kuhusu maisha.

Athari za mazoezi kwenye stress zinakwenda mbali zaidi ya dakika zile unazoshughulisha mwili. Kwanza, mazoezi yanajenga hali ya "kutafakari kwa vitendo."

Unapozingatia jinsi unavyovuta pumzi au hatua unazopiga, akili yako inapata mapumziko kutoka kwenye mawazo hasi yanayoleta stress.

Pili, mazoezi ni adui mkubwa wa ukosefu wa usingizi. Mwili uliochoka kwa mazoezi hupata usingizi mzito na mnono usiku, na kumpa mtu fursa ya kuamka asubuhi akiwa na ubongo uliorejeshwa upya na tayari kukabili siku.

Mwisho, mazoezi huondoa kaza la misuli mwilini, hususan maeneo ya shingo na mabega, ambapo stress hujificha na kusababisha maumivu sugu.

Huhitaji vifaa vya gharama kubwa au kujiunga na "gym" ya kifahari ili uanze kufurahia faida hizi. Kuanza kidogo kwa dakika 30 tu za kutembea kwa haraka, kukimbia taratibu (jogging), au kuendesha baiskeli mara tano kwa wiki kunatosha kabisa kubadili afya ya akili yako.

Usiisubiri stress ikulemee ndipo uanze kukimbia; yafanye mazoezi kuwa ngao yako ya kila siku ya kulinda amani ya akili yako. Anza leo, uujenge mwili wako kuwa ngome isiyopenyeka na msongo wa mawazo.

***Mwandishi ni Ofisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305, Instagram: Emmanuel Jacob***

# Wizara yakwepa...

Inatoka Uk. 23

Mungula alisema madai yaliyotolewa na maseneta hao dhidi ya Tanzania hayana msingi kwani kwa muda mrefu watanzania wamekuwa wakichangamana kidini hadi kufikia hatua ya kuoleana.

Akasema hata tuhuma zinazohusiana na yaliyojiri wakati wa uchaguzi mkuu wa Oktoba waka jana tayari rais Samia Suluhu Hassan alishachukua hatua ya kuunda tume ya uchunguzi na sasa ameunda tume ya kupeleleza kwa kina ili watuhumiwa wachukuliwe hatua stahiki.

Hata hivyo, mbunge huyo akaonya kuwa iwapo serikali haitafanya juhudi kuhakikisha muswada huo hauwi sheria basi Tanzania inaweza kupata madhara makubwa ingawa tuhuma zilizotolewa hazina msingi.

“Vikwazo vitakuwa na madhara sana na itachangia kurudisha nyuma diplomasia ya kiuchumi kati ya nchi zetu hizi mbili,” alisema.

Lakini Nape Nnauye (Mtama-CCM) alishangaa Marekani kwa kupanga kuiwekea vikwazo Tanzania kutokana na mambo ambayo hayahusiani kabisa na nchi hiyo.

Alisema kuwa yaliyotokea wakati wa uchaguzi mkuu ni mambo ya ndani ya nchi ambayo hayapaswi kuingiliwa na nchi nyingine.

“Nchi hii ipo huru, hatukupewa uhuru kama zawadi. Wauheshimu uhuru wetu. Tunaheshimu na tunathamini mchango wao,” alisema Nape ambaye alionekana kuzungumza kwa hamaki kama ilivyo kawaida yake.

Akasisitiza kuwa Tanzania bado inawahitaji marafiki kutoka nje lakini akawaonya kuwa waje lakini wasitumie changamoto ambazo Tanzania inazipitia kuinyanyasa, kuidhalilisha, kuikandamiza na kuionea.

“Wafanye kazi na sisi kwa heshima nidhamu na upendo.

Changamoto za siku moja mbili tatu haziwezi kupima uhusiano wetu na kuwa msingi wa uhusiano wetu,” alisisitiza.

Kisha akawataka watanzania kuilinda na kuitetea nchi yao kwa wivu mkubwa na kamwe wasiruhusu mtu kuwadhalilisha, kuwaonea na kuwanyanyasa na kuwa changamoto walizonazo zisitumike kama fimbo ya kuwachapa.

Kwa upande wake, Mbunge wa Singida Magharibi kupitia CCM, Elibariki Kingu, naye alikanusha tuhuma zilizotolewa na maseneta hao kuwa Tanzania kuna unyanyasaji wa kisiasa na kidini.

Alisema ni Tanzania pekee ambako rais anaweza kwenda kanisani kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti na watu wakachanga bila manung’uniko.

Kingu akalitaka bunge na serikali kufanya kila linalowezekana kuwasiliana na Kamati ya Mambo ya Nje ya Seneti ya Marekani ili kutoa ufafanuzi wa tuhuma zilizomo kwenye muswada huo.

“Inawezekana wamepata habari ya upande mmoja. Fanyeni mpango nendeni mkakae na Kamati ya Marekani. Sisi watanzania tunahitaji Marekani na Marekani inaihitaji Tanzania,” alisema.



Elibariki Kingu

### Waziri ajibu

Ingawa hakuliweka suala hilo kwenye hotuba yake lakini kwa kuwa lilizungumzwa na wabunge wengi tena kwa hisia, Waziri Kombo alilazimika kulitolea ufafanuzi wakati akihitimisha mjadala huo.

Katika ufafanuzi wake Kombo alikubaliana na michango yote iliyotolewa na wabunge kuhusu suala hilo lakini akawataka kutokuwa na wasi wasi na hatua hiyo ya maseneta hao wa Marekani kwani ni utaratibu wa kawaida katika mifumo ya utawala wa nchi hiyo kwa bunge kutoa mapendekezo ya aina yoyote kwa serikali.

Inaendelea Uk.33



Na Rashid MTAGALUKA

# Mabilioni ya miradi sawa, je maisha ya Mtanzania yanabadilika?

WAKATI Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likiendelea kujadili bajeti za serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027, jambo moja limejitokeza wazi; serikali imeendelea kuelekeza nguvu kubwa katika uwekezaji wa miundombinu, huduma za jamii na mageuzi ya kiuchumi yanayolenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Kwa mtazamo wa kwanza, bajeti hizi zinaonesha dhamira ya kuijenga Tanzania ya kisasa yenye reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, huduma za maji na mifumo ya kidijitali.

Hata hivyo, swali muhimu ambalo wananchi wengi wanaendelea kujiuliza ni hili; je, uwekezaji huo mkubwa umeanza kubadili maisha ya Mtanzania wa kawaida?

Katika hotuba mbalimbali za bajeti zilizowasilishwa bungeni, sekta ya miundombinu imeendelea kuwa miongoni mwa walaji wakubwa wa fedha za maendeleo.

Wizara ya Ujenzi pekee imepanga kuendelea kutekeleza miradi mikubwa ya barabara na madaraja huku ikitekeleza maelekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa na Dira ya 2050.)

Hakuna ubishi kwamba uwekezaji huo umeleta matokeo yanayoonekana. Urahisi wa usafiri umeongezeka katika maeneo mengi, gharama za usafirishaji zimepungua katika baadhi ya njia na fursa za biashara zimeongezeka.

Hata hivyo, hoja hapa ni kwamba, mafanikio hayo bado hayajaakisiwa kwa kiwango kikubwa katika mifuko ya wananchi wengi.

Kwa mfano, licha ya ukuaji wa uchumi unaotarajiwa kufikia wastani wa karibu asilimia 6.9 katika kipindi cha muda wa kati, changamoto za ajira hasa kwa vijana bado zinaendelea kujitokeza.

Ukuaji wa uchumi unaonekana zaidi katika takwimu za kitaifa kuliko katika kipato cha kaya nyingi za Watanzania.

Tatizo kubwa linaonekana kuwa ni pengo kati ya ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi. Miradi mikubwa ya maendeleo hujenga msingi wa ukuaji wa muda mrefu, lakini wananchi wanahitaji kuona matokeo ya haraka katika maeneo kama ajira, bei za bidhaa muhimu, mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na upatikanaji wa huduma bora za afya na elimu.

Kwa upande mwingine, serikali imeendelea kusisitiza kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada.

Hii ni hatua muhimu kwa sababu uchumi unaojitegemea huipa nchi uwezo mkubwa wa kupanga na kutekeleza vipaumbele vyake. Hata hivyo, jitihada za kuongeza mapato zinapaswa kwenda sambamba na mazingira rafiki kwa sekta binafsi ambayo ndiyo injini kuu ya uzalishaji na ajira.



Aidha, uchambuzi wa bajeti za mwaka 2026/2027 unaonesha kuwa Tanzania imechagua mkakati wa kujenga kwanza miundombinu na mifumo ya uzalishaji kwa matarajio kwamba manufaa yake yataonekana zaidi katika miaka ijayo.

Huu ni mkakati wenye mantiki ya kiuchumi, lakini mafanikio yake yatapimwa si kwa ukubwa wa fedha zilizotengwa pekee, bali kwa uwezo wake wa kuboresha maisha ya wananchi.

Hatimaye, wananchi hawatapima bajeti kwa mabilioni yaliyoandikwa kwenye vitabu vya Serikali. Watapima kwa uwezo wao wa kupata ajira, kuanzisha biashara, kupata huduma bora za jamii na kumudu gharama za maisha. Hapo ndipo mafanikio halisi ya bajeti ya 2026/2027 yatakapoweza kuonekana.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

## Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

# Tumechoshwa na ahadi ya Tanesco

**Mhariri,**
SISI wananchi wa Kata ya Kigogo Fresh B, Mtaa wa Golani tuna changamoto ya umeme na tulifuatilia tangu mwaka 2024 na mwaka 2025 ikatengwa bajeti inayoisha Juni 2026 lakini hadi sasa hakuna dalili yoyote.

Hadi sasa ni nyumba takriban 200 hazijafungiwa nishati hiyo ya umeme na kila tukifuatilia tunaambiwa tusubiri. Sasa tumechoka kusubiri.

**Ni sisi wakazi wa Kata ya Kigogo Fresh B**

# Hospitali ya Mwananyamala iongezewe madaktari

**Mhariri,**
KUMEKUWA na foleni ndefu ya kuona madaktari katika Hospitali ya Mwananyamala, iliyoko Kinondoni, Dar es Salaam. Inaonyesha wazi kwamba hospitali hii ina upungufu mkubwa wa madaktari kwani wagonjwa ni wengi sana na wakati mwingine baadhi ya wagonjwa wamekuwa wakizidiwa wakiwa kwenye mabenchi ya kusubiri huduma.

Inashangaza kuwa ni vyumba viwili tu ndiyo vinavyotumika kuwahudumia wagonjwa, jambo linaloonyesha kuwa kuna uhitaji mkubwa wa madaktari.

Tunaiomba serikali ifanye hima juu ya changamoto hii katika Hospitali ya Mwananyamala.

**Ezekiel Urio,**
**Kinondoni, Dar es Salaam.**

# Watumiaji SGR tuwe wastaarabu

**Mhariri,**
MIMI ni mmoja watumiaji wazuri wa usafiri wa treni ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Nimeanza kupatwa na wasiwasi kuhusiana na uharibifu wa miundombinu ninaoushuhudia ndani ya mabehewa ya treni hiyo ya kisasa.

Mathalan, hivi sasa viti vingi havina vile vifaa vya kuwekea chupa za maji vinavyokuwa nyuma ya siti kwa sababu vimeng'olewa na abiria wasio wastaarabu.

Kuna baadhi ya meza za kuwekea vitu vidogo vidogo zimeanza kulegea na huenda baada ya muda zitaanza kung'oka.

Hii yote inatokana na matunzo hafifu yanayofanywa na baadhi ya abiria.

TRC inajitahidi sana kutoa matangazo kuwahimiza abiria kuvitumia vifaa hivyo ipasavyo, lakini pamoja na kufanya hivyo, nashauri pia waanze kuweka uangalizi wa kutosha dhidi ya baadhi ya abiria wasio wastaarabu.

Pia nashauri waanze kuvifanyia ukarabati vifaa vilivyoharibiwa.

Iwapo TRC itadharau kufanya ukarabati huo hivi sasa, basi baada ya muda mabehewa mengi yatakuwa katika hali mbaya na wakati huo ukarabati wake utaigharimu fedha nyingi.

**Juma Akida,**
**Mbezi Luis,**
**Dar es Salaam.**

# Migiro: CCM tunaguswa sana na utekaji

Na Mwandishi WETU

BAADA ya wanaharakati pamoja watu kwenye mitandao ya kijamii kushutumu Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa kukaa kimya kuhusu matukio ya utekaji na watu kupotea, hatimaye katibu mkuu wa chama hicho, Dkt. Asha-Rose Migiro amefunguka.

Dkt. Migiro amesema CCM inaguswa kwa ukaribu mkubwa na kadhia hiyo kwani hata wanachama wake wenyewe wamekuwa wahanga wa vitendo hivyo.

Katibu mkuu huyo wa chama tawala, alitoa kauli hiyo wiki iliyopita wakati akifanyiwa mahojiano na chombo kimoja cha habari hapa nchini.

"Msimamo wa CCM uko wazi na hauwezi kamwe kuunga mkono au kufumbia macho utekaji unaoendelea nchini," amesema.

Dkt. Migiro amezungumzia pia kuhusu kukosekana kwa uwajibikaji kuhusu mauaji ya Oktoba 29,2025, akisema suala la uwajibikaji lina nafasi kubwa sana ndani ya CCM na serikali yake, na kwamba msimamo wa mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan, uko wazi kuwa "hakuna mtu aliye juu ya sheria."

Akizungumzia kuhusu madai ya Jeshi la Polisi kukilinda na kutetea chama tawala dhidi ya vyama vya upinzani, amesisitiza kuwa jeshi hilo ni chombo cha kitaifa chenye wajibu wa kulinda raia wote bila kujali itikadi zao za kisiasa.

"Hata mchakato mzima wa kampeni za uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2025, ulienda kwa utulivu mkubwa nchi nzima, jambo linalothibitisha kuwa vyombo vya ulinzi havikuingilia wala kukandamiza haki za raia kwa niaba ya CCM," amesema Dkt. Migiro katika mahojiano na chombo kimoja cha habari jijini Dar es Salaam.

Aidha, amefafanua sababu zilizoifanya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya chama hicho, kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatia matukio ya ghasia za Oktoba 29, 2025, akisema kuwa kazi ya ziada iliyofanywa na majeshi hayo ndiyo iliyookoa nchi kuingia kwenye maafa makubwa zaidi.



Dkt. Asha-Rose Migiro

Dkt. Migiro amesisitiza kuwa CCM inaendelea kuonesha masikitiko yake makubwa kwa vifo vya Watanzania 518 vilivyothibitishwa na Tume ya Jaji Othman Chande, akieleza kuwa kwa chama tawala, uhai wa mtu mmoja ni jambo zito lisiloweza kupimwa kwa namba.

Vilevile alikiri kuwa matukio ya ghasia na maafa yaliyotokea katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025 yalilishtua taifa zima na kuwaduwaza wana-CCM kuliko mtu mwingine yeyote.

Dkt. Migiro ameweka wazi msimamo rasmi wa chama hicho, akisema kuwa CCM imeipokea kwa umakini mkubwa Ripoti ya Jaji Othman Chande na inataka kuona hatua madhubuti zikichukuliwa ili kuhakikisha dhoruba hiyo haijirudii tena nchini.

Mtendaji huyo mkuu wa CCM, amesema chama hicho tawala kilichukua muda wa kuzungumza kwa kina kwa kuwa ilihitajika nafasi ya kutafakari kisababishi cha nchi kupoteza utulivu wake wa kihistoria baada ya miaka mingi ya amani na mshikamano.

Habari

# Msigwa: Adui yetu mkubwa ni ukosefu wa haki



Na Mwandishi WETU

WIKI chache baada ya aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa kutangaza kurejea Chadema, amefunguka akisema kuwa adui mkubwa hapa nchini hivi sasa ni ukosefu wa haki.

Septemba 8, 2024, Mchungaji Msigwa alikiri kwa kinywa chake kwamba alikuwa mjinga alipokuwa Chadema na kwamba hakuuona ujinga huo hadi aliporejea CCM kwa kupokelewa na wajumbe wa mkutano wa halmashauri kuu ya chama hicho tawala.

Alikabidhiwa kadi ya chama hicho na mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan.

Mwanasiasa huyo machachari ambaye pia alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, alitangaza kurudi ndani chama chake hicho cha zamani Mei 23, 2026 baada ya kuachana na CCM.

Wiki iliyopita uongozi wa Chadema Jimbo la Iringa Mjini, uliitisha mkutano maalum wa bodi ya chama kwa ajili ya kumkaribisha Msigwa pamoja na wanachama wengine wapya na wale waliorejea ndani ya chama hicho.

Akizungumza mbele ya viongozi na wanachama, Msigwa aliomba radhi kwa dhati kwa changamoto au sintofahamu zozote zilizowahi kujitokeza hapo awali.

Pamoja na mambo mengine alisisitiza umuhimu wa umoja, mshikamano na ushirikiano ndani ya chama ili kufanikisha ushindi na kuleta mabadiliko ya kweli kwa wananchi.

“Pamoja na changamoto ambazo naweza nikasema nina sababu ya kujitetea hadi nikafanya maamuzi ya kuhama, hazina mashiko nilipaswa niamue tofauti…”

“Unajua ukiwa kwenye nyumba yenye dari halafu imeshika moto, watu walioko chini hawaoni moto  ukiruka ukadondoka chini watu watakulaumu kwanini uliruka…kwa hiyo lawama utapewa wewe…”

“Hivyo wote wanaonipinga, wanaotukataa, wanaotupokea wote mimi naona wana haki kwa sababu ule moto walikuwa hawauoni lakini hiyo sio sababu sasa ya kusema turudishe yale mambo ya zamani,”amesema Msigwa.

Anasema alitakiwa kutulia na kuendelea kupambana lakini kwa kuwa yameshatokea ndiyo maana akaomba msamaha.

“Na sijaja hapa au sijarudi Chadema kwa sababu nataka cheo, sijaja hapa kuleta makundi, adui yetu mkubwa ni umaskini, adui yetu mkubwa ni magonjwa, adui yetu mkubwa ni ujinga…”

“Lakini adui mkubwa zaidi ni ukosefu wa haki katika taifa hili, adui mkubwa kabisa katika taifa letu la Tanzania ni mifumo ambayo imefeli kufanya kazi, tujenge siasa za hoja wananchi wanataka siasa za hoja ambazo zitawasaidia,”amesema Mchungaji Msigwa.

Kwa upande wake, Katibu Mwenezi wa Chadema Jimbo la Iringa Mjini, Oscar Mgaya, alimpongeza Msigwa kwa kurejea Chadema kuendeleza mapambano.

Mgaya aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea kudumisha umoja, mshikamano na msimamo thabiti kwa maslahi ya chama.

# Msigano mkali Msajili, Chadema




**Na Mwandishi WETU**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini pamoja na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) wapo kwenye msigano mkali wa kisheria.

Msigano huo umetokana na hatua ya Msajili kuiandikia Chadema barua ya pili ikikitaka chama hicho kujielezea kwa nini kisiadhibiwe kutokana na kukiuka sheria.

Siku chache baada ya Mahakama "kumpiga kufuli" Msajili kuadhibu Chadema kutokana na tuhuma alizozielekeza kwa chama hicho, Msajili ameibuka na barua nyingine inayofanana na ile ya kwanza, akitishia kukisimamisha au kukitoza faini chama hicho endapo hakitatoa majibu ya kuridhisha kutokana na kukiuka sheria ya vyama vya siasa.

Barua ya kwanza iliyosainiwa na Naibu Msajili, Sisty Nyahoza iliandikwa Mei 7, 2026 ambayo ilikuwa ikikitaka Chadema kijieleze kutokana na baadhi ya wanachama wake kukiuka utekelezaji wa masharti ya sheria ya vyama vya siasa Sura ya 258 na urekebu la mwaka 2023 wakiwa katika shughuli za chama chao.

Mei 29, 2026 Nyahoza aliandika barua nyingine kwenda Chadema akikitaka kuwasilisha maelezo kuhusu utekelezaji wa masharti ya sheria ya vyama vya siasa Sura ya 258 toleo la urekebu la mwaka 2023 wakiwa katika shughuli za chama chao.

Barua hiyo imewataja wanachama wa chama hicho, Joseph Mbilinyi (Sugu) pamoja na Samwel Welwel kwamba kwa nyakati tofauti waliongea maneno ambayo yanakiuka sheria hiyo ya vyama vya siasa.

Baada ya barua hiyo kusambaa katika mitandao ya kijamii, wadau wa siasa, wanaharakati na wanasheria waliibuka wakihoji uhalali wa Msajili kuiandikia Chadema barua nyingine wakati tayari kuna zuio la Mahakama Kuu ya Tanzania, Masjala Ndogo ya Babati mkoani Manyara la Mei, 25, 2026.

Katika uamuzi mdogo wa maombi ya Namba 12812 ya 2026 yaliyofunguliwa na Katibu mkuu wa Chadema pamoja na Bodi ya Wadhamini ya kupatiwa kibali cha kufungua maombi ya kupata amri ya kukataza au zuio.

Mwanasheria nguli, Mpoki Kaba, aliandika kwenye ukurasa wake wa X - zamani twitter - kuwa katika mfumo wowote wa sheria, kanuni ya kutii amri za mahakama ndiyo kiini cha utawala wa sheria.

Alisema athari za kutotii amri hizo haziishii kwenye kesi za mtu mmoja mmoja pekee bali zinatishia uadilifu na uthabiti wa mfumo mzima wa sheria.

"Amri za mahakama siyo mapendekezo ya kawaida, bali ni maagizo ya lazima yaliyowekwa kwa ajili ya kutatua migogoro, kudumisha utulivu wa umma na kulinda haki, kutotii amri hizo ni kunadhoofisha mfumo wa mahakama na kuvuruga mizania nyeti ya utawala," amesema Wakili Mpoki.

Inaendelea Uk.32

■ Habari

# Msigano mkali...

Inatoka Uk. 31

Katikati ya mjadala huo, Nyahoza alionekana kwenye picha mjongeo akitolea ufafanuzi suala hilo, akisema kuwa zuio lililowekwa na mahakama halina uhusiano na barua hiyo mpya aliyoiandika kwa Chadema.

"Barua ambayo tumewaandikia Chadema tarehe 26 Mei, 2026, kuwataka wawasilishe maelezo kuhusu ukiukwaji wa sheria zilizofanywa na viongozi wao akiwemo Joseph Mbilinyi (Sugu), kwa maneno ambayo aliongea jukwaani ambayo ni matusi na dhihaka.

"Kuna watu wanasema sisi kuwaandikia barua Chadema tarehe 26 Mei imekiuka amri ya mahakama ambayo imetuzuia kukichukulia hatua chama hicho kutokana na barua tuliyowaandikia tarehe 7 Mei mwaka huu.

"Zuio la mahakama linahusu barua yetu ya tarehe 7 Mei, 2026 na haijatuzuia sisi tusifanye kazi yetu katika kusimamia vyama vya siasa. Sisi tunaendelea na kazi yetu na ndiyo maana tumewaandikia barua nyingine tarehe 26 Mei, 2026 pale tulipoona kwamba kuna ukiukwaji wa sheria, kwa hiyo zuio la mahakama halihusiani na ile barua ya tarehe 26, Mei.

"Mfano ni kama mtu unamiliki duka, halafu unamiliki shule, kuna mtu unamdai pale dukani kwako amekopa na kule shuleni hajalipa ada ya mwanaye, sasa akienda mahakamani akiomba usimdai deni la dukani, haina maana usimdai na deni la ada ya mwanaye. Hivi ni vitu viwili tofauti," alisema Naibu huyo msajili wa vyama vya siasa.



*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa kikao cha kupokea Taarifa ya Sensa ya Wanyamapori iliyofanyika nchi nzima mwaka 2024 – 2025 iliyowasilishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Ashatu Kijaji, Ikulu Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu).*

# Wizara yakwepa...

Inatoka Uk. 26

"Kwa mfumo wa Marekani Legislative (Bunge) lina mamlaka ya kutoa pendekezo lolote. Linaweza kupendekeza kumfungia mtu, kumfungia rais, kumfungia mjomba, kumfungia shangazi. Lina haki hiyo," alisema.

Aliwahakikishia wabunge kuwa wizara yake italifanyia kazi haraka iwezekanavyo pendekezo la wabunge kutaka Bunge la Tanzania kuwasiliana na seneti ya Marekani kuhusiana na suala hilo.

"Haiwezekani maisha sisi tuwe tunasemwa tu, tunasemwa tu… hoja hujibiwa kwa hoja. Na sisi tunataka kujibu kwa mujibu wa sera yetu, kirafiki, kwa upole na kwa amani. Ulezi wote aliotupa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere sisi ndiyo tunataka kwenda nao,"alisema.

Akaliambia bunge kuwa kwa kuwa Bunge hujibiwa na Bunge, basi kupitia michango yao wabunge walikuwa wametoa majibu kwa Bunge la Marekani linalopanga kutunga sheria hiyo dhidi ya Tanzania.

Akasema wizara yake itayaandika yale yote yaliyozungumzwa na wabunge kama sehemu ya majibu ya wizara hiyo kwa hoja iliyopelekwa Seneti na wanasiasa hao wawili.

"Na bahati nzuri serikali ya Marekani imeleta wawakilishi wake hapa leo, wapo pale juu. Tena wameleta waswahili wenzetu kwa hiyo naamini watafikisha haya yaliyosemwa neno kwa neno," alisema.

**Hoja yenyewe iliyoko Seneti**

Mjadala huo umetokana na hatua ya maseneta wawili wa Marekani, Jeanne Shaheen kutoka chama cha Democrat jimbo la New Hampshire na Ted Cruz, mwanachama wa Republican kutoka Texas, kupeleka muswada unaolenga kutunga sheria ya kuiwekea vikwazo Tanzania kutokana na tuhuma za ukiukwaji wa haki za kisiasa na unyanyasaji wa kidini.

Muswada huo unapendekeza hatua mahususi na kali za kuchukuliwa dhidi ya Tanzania iwapo haitajirekebisha.

Unampa mamlaka rais wa Marekani kuweka vikwazo ikiwamo kuzuia visa na rasilimali dhidi ya watanzania watakaobainika kujihusisha na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.




*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba, akiangalia ubanguaji wa korosho wakati alipotembelea mradi wa mnyororo wa thamani wa Korosho kupitia Kiwanda Darasa cha Kubangua Korosho (KIDAKUKO) cha CAMARTEC kilichopo Masigati wilayani Manyoni, mkoani Singida, mwishoni mwa wiki.(Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)*

Habari

# Waandishi wahimizwa kupaisha BIG-Z

Na Mwandishi MAALUM

WAANDISHI wa habari Zanzibar wametakiwa kuwa daraja la kuelimisha jamii kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Ukuaji Jumuishi wa Kiuchumi Zanzibar (BIG-Z).

Elimu inayohimizwa ni kuhusu masuala ya uhamishaji, uthamini wa mali na ulipaji fidia kwa wananchi watakaoathirika na mradi huo.

Mwito huo umetolewa na Kiongozi wa Ufuatiliaji wa Mpango wa Uhamishaji Watu na Makazi, Dkt. Mussa Mhagama (pichani), wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi za Mradi wa BIG-Z, Mbweni, Zanzibar kuhusu mwenendo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango wa uhamishaji na fidia kwa waathirika wa mradi.

Dkt. Mhagama alisema vyombo vya habari vinaaminika na jamii, hivyo waandishi wana nafasi kubwa ya kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi kuhusu hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo, ikiwemo taratibu za uthamini, vigezo vya malipo ya fidia na namna mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko unavyofanya kazi.

Alisema serikali inatekeleza mradi huo kwa kuzingatia sheria, taratibu na viwango vilivyoidhinishwa, huku kila hatua ikifuatiliwa kwa karibu ili kuhakikisha wananchi wanaostahiki fidia wanapata haki zao kwa uwazi, usawa na kwa wakati.

"Ni muhimu wananchi wakaelewa kuwa mradi huu una mfumo rasmi wa kupokea na kushughulikia malalamiko. Wanapokutana na changamoto, wanapaswa kuutumia mfumo huo ili kupata ufumbuzi kwa wakati badala ya kubaki na sintofahamu," alisema Dkt. Mhagama.

Aliongeza kuwa tathmini ya awali inaonesha wananchi wengi katika maeneo yanayopitiwa na mradi tayari wana uelewa mzuri kutokana na elimu na uhamasishaji uliotolewa kabla na wakati wa kuanza kwa utekelezaji wake.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini, Protas Benedict Sayo, alisema jukumu la timu yao ni kufuatilia viashiria mbalimbali vinavyoweza kusaidia mradi kufikia malengo yake, huku ukileta matokeo chanya kwa jamii na kupunguza athari zisizohitajika.



Sayo alisema kupitia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini uliowekwa, timu hiyo hukusanya taarifa kutoka kwa waathirika wa mradi, viongozi wa maeneo husika na wadau wengine wa maendeleo, ili kutathmini mwenendo wa utekelezaji na kuhakikisha haki inapatikana kwa kila anayestahiki.

Alifafanua kuwa kiwango cha fidia hutegemea aina na ukubwa wa athari iliyopatikana, hivyo si lazima kila mwananchi alipwe kiwango kinachofanana. Kila mmoja hulipwa kulingana na tathmini iliyofanyika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Mradi wa BIG-Z unaotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, unalenga kuimarisha maisha ya wananchi kupitia uboreshaji wa miundombinu, huduma za kijamii na maendeleo jumuishi ya kiuchumi.

Kupitia mradi huo, wananchi wa maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba watanufaika na miradi ya barabara, mitaro ya maji, usimamizi wa taka na uboreshaji wa mazingira ya makazi, huku mpango wa uhamishaji na fidia ukipewa kipaumbele ili utekelezaji wake uwe wa haki, uwazi na wenye kuzingatia maslahi ya jamii.

# Bunge laipongeza Serengeti Boys

**Na Hellen NGOROMERA**




BUNGE la Tanzania limepitisha azimio la kuipongeza timu ya vijana wanaume wenye chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Boys, kwa kutinga fainali za michuano ya mabingwa wa soka Afrika (Afcon).

Pia, Serengeti Boys imekata tiketi ya kushiriki mashindano ya kombe la dunia la vijana chini ya umri wa miaka 17 baadaye mwaka huu.

Akiwasilisha hoja hiyo bungeni, Mbunge wa Bunda Mjini, Esther Bulaya, amesema ushindi wa Serengeti Boys na hatua waliyofikia kimichezo ni jambo kubwa na la kihistoria ambalo halijawahi kutokea hapa nchini kwa muda mrefu.

"Wote tumeshuhudia tarehe 28 Mei, 2026, timu hii ya Serengeti Boys ikipata ushindi dhidi ya Timu ya Taifa ya Vijana ya Misri katika mchezo wa nusu fainali…"

"Timu yetu ilishinda kwa mikwaju ya penati 4 kwa 3 baada ya timu zote kutoka suluhu ya bila kufungana hadi mwisho wa mchezo huo uliofanyika nchini Morocco," amesema Bulaya.

Ameeleza kuwa kwa matokeo hayo, Serengeti Boys wameingia fainali za mashindano hayo, lakini pia timu hiyo imekata tiketi ya kushiriki mashindano ya kombe la dunia kwa vijana wa chini ya umri wa Miaka 17 yanayotarajiwa kufanyika nchini Qatar.

"Timu hili inapaswa kupongezwa na kupewa moyo, ari na hamasa kutoka kwa Watanzania wote tukiwemo sisi wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi…"

"Kufuzu kwa timu hiyo katika mashindano hayo ni fursa kubwa ya kuitangaza Tanzania

kimataifa na kuitangazia dunia kuwa sisi ni nchi ya amani na kwa njia hiyo kukuza utalii na uwekezaji nchini," amesema Bulaya.

Ametoa pongezi kwa serikali kwa kuimarisha sekta ya michezo kupitia uwekezaji mkubwa ambao unaleta motisha kubwa kwa vijana na wanamichezo kwa ujumla kuongeza juhudi za ushiriki katika mashindano mbalimbali.

Wakichangia hoja hiyo wabunge wamesifu na kupongeza juhudi za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuinua na kuhamasisha sekta ya michezo nchini.

Mbunge wa Viti Maalumu wa mkoa wa Tanga, Husna Sekiboko (CCM), amesema matokeo ya timu hiyo ya vijana yameitangaza Tanzania dunia nzima na kwamba matokeoa hayo yametokana na juhudi na jitihada na utayari wa serikali katika kuwekeza katika sekta ya michezo.

"Rais Samia amekuwa na utayari kuwekeza katika ujenzi wa viwanda lakini amewekeza katika akademia za michezo. Zamani tulikuwa tunaona watu wanapiga kelele kwa nini tusilee vipaji vya watoto wakiwa wadogo," amesema.

Ameeleza kuwa ndani ya miaka mitano zimefunguliwa akademia za michezo katika maeneo mbalimbali kukiwemo Kigamboni Dar es Salaam, mkoani Tanga na kwingineko nchini.


Naye mbunge wa Jimbo la Makete, Festo Sanga (CCM), amesifu jitihada za Rais Samia kuhamasisha sekta ya michezo nchini akisema hayo ni mafanikio makubwa pia amempongeza Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Paul Makonda kwa juhudi anazozionyesha katika kusimamia wizara anayoiongoza.

# Marathoni


MAC D
MARATHON
2026
MARATHON
MAC D
KUNDUCHI
MARATHON
4TH JULY, 2026
NDC GROUND KUNDUCHI
Jisajili sasa
35,000Tsh.
www.macdmarathon.com
KWA MSAADA PIGA : 0719 799 848 | 0702 562 009
NHC
BUILDING OUR NATION
EB MARITIME GROUP
Total Logistics Network
KILIMANJARO
NATURAL MINERAL WATER
TANZANITE
Royal Gin
AZANIA BANK
KALUBA
Let's Connect
montage
ITV
RADIO One
ayo TV
RBS
BUILDERS & CIVIL WORKS
4J'S FITNESS center
www.4jsfitnesscenter.co.tz

# Jinsi ya kusoma Pambazuko





Na Anti MSHAURI





# Wanaume wasinyanyase wake zao

NI wiki nyingine tena tunakutana kupitia safu hii kwa lengo la kupeana maarifa kuhusiana na masuala mbalimbali ya maisha.

Wiki hii nitazungumza namna wanaume wanavyopaswa kutunza wake zao.

Ndoa ni ushirika kati ya mume na mke ambao wanapaswa kusaidiana masuala mbalimbali ya kifamilia. Ndoa inapaswa kulindwa kwa nguvu zote ili kuhakikisha kuwa shirika huu unaleta matunda yaliyokusudiwa.

Mwanaume anapaswa kumpenda na kumheshimu mkewe. Ndoa inataka heshima na si unyanyasaji hivyo mume anapaswa kuwa nguzo kuu kwa mkewe.

Katika maisha ya hivi sasa ndoa nyingi zimekuwa zikivunjika au kuyumba na sababu kuu ikiwa ni wanaume kukosa uaminifu kwa wake zao.

Kukosa uaminifu kwa wanaume hao kumesababisha wake zao kupata maumivu na matatizo mengine; hali ambayo inasababisha familia kuyumba na kuporomoka.

Mwanaume anapaswa kumpenda mkewe kwa matendo na si maneno pekee kwa kumsaida majukumu machache ya nyumbani kwani hali hiyo huimarisha upendo kati yao.

Anapaswa pia kukwepa unyanyasaji wa aina yoyote kwani unyanyasaji si kupiga ngumi pekee bali hata kumfanya awaze mambo unayomfanyia na kumfanya ajione hana thamani lakini pia unyanyasaji unaweza kuwa wa kumzuia kutofanya kazi (ikiwa ana taaluma ya kitu fulani) au kumnyima fedha na mambo mengine.

Lakini pia kuachana na usaliti kwa kuepuka vitendo vya kuchepuka kwani kwa kiasi kikubwa vikijulikana na mke ndivyo vinaleta malumbano na mfarakano kwenye ndoa.

Mwanaume kumbuka kuwa mwanaume hodari ni yule anayelinda ndoa yake na siyo yule anayechapa mke hivyo anapaswa kujenga na si kubomoa.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***



# Gauni lililotengenezwa kwa mikate latikisa tuzo za filamu Afrika

HAFLA ya tuzo za Afrika Magic Viewers Choice Awards ambayo mwaka huu imefanyika nchini Nigeria, iligeuka kuwa tamasha la mitindo badala ya sherehe ya tuzo.

Hafla hiyo ilifanyika hoteli ya Eko and Suites, mjini Lagos, ilihudhuriwa na watu maarufu pamoja na watengenezaji wa filamu.

Katika maonyesho ya mavazi, Queen Mercy Atang ambaye ni nyota wa kipindi cha TV, aliwashangaza wengi baada ya kuvaa vazi lililovutia zaidi usiku huo, kwa kuvaa gauni lililotengenezwa na mikate zaidi ya 500.

Akiwa amezungukwa na wasichana wawili waliobeba sahani za mikate na wasaidizi kadhaa waliomsaidia kubeba mavazi hayo makubwa kupitia zulia jekundu, Atang alionekana akiwa na ugumu wa kutembea kwa uhuru.

Akizungumza na vyombo vya habari, alisema mavazi hayo yalibuniwa kutangaza biashara yake ya uokaji mikate huku akisisitiza kuwa muonekano huo ulikuwa mkakati wa makusudi wa masoko badala ya kutafuta tu usikivu wa watu.

“Ni sehemu gani bora zaidi ya kutangaza biashara yangu kuliko Africa Magic Viewers’ Choice Awards?” alisema.

Gauni hilo lilibuniwa na mbunifu mashuhuri Toyin Lawani wa Tiannah’s Empire, ambaye alitoa maoni kwenye Instagram akisema anaanzisha mtindo wa “kila mtu kuvaa biashara yake.”

Muonekano huo uligeuka mara moja kuwa mojawapo ya mada kubwa zaidi kwenye mitandao ya kijamii usiku huo.

# Manjano, maziwa kiboko ya weusi kwapani

SEHEMU kamass kwapa na katikati ya mapaja huwa zinaongoza kwa kupata weusi.

Wapo pia ambao hupata weusi katika sehemu tofauti kama chini ya macho, nyuma ya magoti na kadhalika.

Leo nimekuwekea namna bora ya kuondoa hali hiyo kwa kutumia maziwa fresh na manjano.

Maziwa yana sifa ya kung’arisha ngozi na manjano husafisha ngozi.

* Chukua maziwa vijiko viwili na manjano kiasi cha kutengeneza uzito wa mchanganyiko huo kisha pakaa sehemu iliyoathirika na weusi.

Tumia pamba na usugue taratibu, baada ya muda kidogo nawa na endelea na huu utaratibu kila siku unapopata muda. Utapata matokeo mazuri.





# Wimbo wa Shakira Kombe la Dunia wakosolewa

Na Mwandishi WETU

WIMBO mpya wa Kombe la Dunia 2026 unaoitwa Dai-Dai kutoka kwa Shakira akimshirikisha Burna Boy, umekosolewa mitandaoni huku mashabiki wengi wakilinganisha na wimbo maarufu wa kombe hilo mwaka 2010 Waka Waka (This Time for Africa).

Wimbo huo umetolewa ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea michuano ya Kombe la Dunia 2026 na tayari umevuta hisia kubwa kutoka kwa mashabiki wa soka na muziki duniani kote.

Video ya "Dai Dai" imehusisha mastaa wakubwa wa soka akiwemo Lionel Messi, Kylian Mbappé, Vinícius Júnior, Erling Haaland pamoja na Alexia Putellas.

Video hiyo imejaribu kuonesha umoja wa tamaduni mbalimbali kupitia burudani, dansi na mazingira ya viwanjani yaliyojaa shamrashamra za soka.

Mashabiki wengi mtandaoni wamekosoa video hiyo huku wengi wakisema imejaa matumizi makubwa ya CGI na mandhari za green screen zilizofanya ionekane ya kutengenezwa kupita kiasi.



# Rhino alaumu wimbo wa Rayvanny

Na Mwandishi WETU

MSANII wa muziki wa Injili na aliyekuwa mwanachama wa kundi la The Mafiki, Rhino King, amemshushia lawama msanii wa Bongo Fleva, Rayvanny, akidai wimbo wake mpya unachochea vijana kubeti badala ya kuelimisha jamii. Rhino amedai kuwa kwa ukubwa wa Rayvanny, hakutarajia kuona akisajili nguvu yake kwenye nguzo inayohamasisha mchezo wa kamari.

Baadaye Rayvanny mwenyewe alimjibu Rhino kupitia ukurasa wake wa Instagram akiandika; "Kaliwa kamari anamaliza hasira kwangu" akimaanisha kuwa Rhino ameliwa baada ya kubeti na sasa anatafuta mchawi.

# Arsenal yaiamsha 'roho ya Raila'

Na Mwandishi WETU

KIFO cha Raila Amolo Odinga hakijazima nafasi yake katika mioyo ya Wakenya.

Kinyume chake, kimeonyesha namna kiongozi anaweza kuendelea kuishi ndani ya kumbukumbu za watu, siyo kwa hotuba tu alizowahi kutoa, bali pia kwa mambo madogo yaliyomfanya aonekane wa kawaida; kwa watu na mwenye hisia kama wao. Moja ya mambo hayo ni mapenzi yake makubwa kwa Arsenal.

Wiki iliyopita, wakati Arsenal ya England ilipotwaa ubingwa wa ligi kuu ya nchi hiyo baada ya kusubiri kwa muda mrefu – miaka 22, furaha hiyo haikuishia London pekee. Nchini Kenya, hasa Jiji la Nairobi, mashabiki wengi walifunga mitaa na barabara, wakiimba, wakishangilia na kumkumbuka Raila kama mmoja wao.

Kwao, ushindi wa Arsenal haukuwa tu ushindi wa klabu ya soka; ulikuwa pia zawadi ya kihisia kwa Raila ambaye huitwa "Baba."

Kwa shangwe hizo za Wakenya kufurahia ushindi wa Arsenal, ndipo kunajengeka dalili zote kwamba soka huvuka mipaka ya mchezo. Kwamba kabumbu ni siasa na maisha yasiyojali mipaka.

Soka pia ni lugha ya kumbukumbu, upendo na utambulisho. Wakenya walipokuwa wakiimba nyimbo za kumsifu Raila, walikuwa wakisema jambo kubwa zaidi; kwamba hata katika kifo, kiongozi huyu hakuwa mbali nao.

Kwamba Raia anaendelea kuwa sehemu ya mijadala yao ya kisiasa, maisha yao ya kila siku na hata utani wao wa soka. Alikuwa mwanasiasa mkubwa, lakini pia shabiki aliyeweza kuumia Arsenal inapofungwa na kushangilia inaposhinda.

Safari ya baadhi ya wananchi kwenda Bondo, alikozikwa, "kusheherekea" naye ubingwa huo inaonyesha kina cha uhusiano kati ya Raila na wafuasi wake.

Kwa kawaida, kaburi ni mahali pa huzuni, lakini kwa tukio hili, Bondo iligeuka kuwa uwanja wa kumbukumbu, shukrani na mazungumzo ya kimya kati ya walio hai na marehemu waliyempenda.






Kisiasa, tukio hili lina maana kubwa. Linaonyesha kuwa urithi wa Raila haukujengwa na uchaguzi pekee, bali na uhusiano wa kiroho na kijamii alioujenga kwa wananchi. Alikuwa alama ya upinzani, matumaini, uvumilivu na ndoto zisizokufa.

Ndiyo maana Arsenal iliposhinda, Wakenya wengi hawakusema tu "tumeshinda." Walisema, kwa hisia nzito; "Baba, umeona?" Huo ndio ushahidi kwamba Raila bado yupo — katika nyimbo, katika machozi, katika mitaa, na sasa, hata katika furaha ya Arsenal.



# Wenger aitabiria makubwa Serengeti Boys

## Inachuana kesho na Senegal fainali



Na Yassin LUPATU

TIMU ya Taifa ya Vijana Tanzania – Srengeti Boys, kesho inaingia uwanjani kumenyana na Timu ya Senegal katika Fainali za Mabingwa wa Soka Afrika chini ya miaka 17.

Serengeti Boys ambao wameingia fainali za soka za michuano mikubwa Afrika kwa vijana (AfconU17) baada ya kuichabanga Misri kwa mikwaji ya penati 4-3, inakuwa timu ya kwanza Tanzania kufikia hatua hiyo kubwa. Mchezo wao utachezwa katika Uwanja wa Moulay El Hassan Stadium iliyoko mjini Rabat, nchini Morocco.

Inaelezwa na wataalamu wa soka kwamba Tanzania inaweza kuibuka kidedea kwa kuwa wachezaji wa Serengeti Boys wanabebwa na nidhamu, wepesi, mashambulizi dhidi ya adui uwanjani kama walivyodhihirisha wakati wa mchezo wao wa nusu fainali na Misri.

Mmoja wa watu mashuhuri duniani ambaye alifurahishwa na mchezo wa Serengeti Boys ni Arsène Wenger ambaye ni mshauri na bingwa wa mikakati ya soka duniani. Hivi sasa ni Mkuu wa Maendeleo ya Soka Duniani katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA) na kocha wa zamani wa Arsenal.

Kimsingi, Wenger anaeleza kuwa Tanzania ina vipaji, uwezo upo, lakini mafanikio ya kudumu yatazaliwa tu kama soka la vijana litapewa uzito wa kitaifa.

Wenger alisema Tanzania imeonyesha kiwango cha juu cha mpira na anatarajia kuwaona vijana hawa wakifanya vyema zaidi mbele ya safari.

Zaidi ya hapo, anaamini Serengeti Boys wanaweza kufika katika Kombe la Dunia la vijana chini ya miaka 17. Hii ni sifa kutoka kwa mtu aliyelitazama soka kwa macho ya kiwango cha juu kwa miongo kadhaa.

Lakini pongezi hizi pia zinapaswa kuibua tafakuri. Pamoja na maandalizi yasiyoridhisha na hamasa hafifu kwa Watanzania kuibeba timu hii, vijana wamefanya makubwa. Hili linaonyesha kuwa Tanzania ina dhahabu ya soka, lakini bado haijajenga kiwanda madhubuti cha kuisafisha, kuilinda na kuipeleka sokoni.

Kama vijana hawa wangeandaliwa kwa mpango mpana zaidi, kwa michezo mingi ya kimataifa, vifaa bora na uangalizi endelevu, huenda tungekuwa tunazungumza lugha kubwa zaidi.

Sasa ni wakati wa kuwekeza katika akademi, makocha bora, lishe, sayansi ya michezo, mashindano ya vijana, viwanja na ufuatiliaji wa vipaji kuanzia shule hadi klabu.

Serengeti Boys wametuma ujumbe; Tanzania inaweza. Sasa kinachohitajika ni mfumo utakaofanya mafanikio haya yasiwe tukio la bahati, bali mwanzo wa zama mpya za soka la Tanzania.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION